Jamii

**Mwendokasi isiwe adhabu kwa maskini wa Mbagala**

Uk. 23

Michezo

**Hersi kutimiza ahadi zake?**



Uk. 42

Mzee Tai



**Wajipange, Nchimbi hana uzito wa unyoya kwenye siasa**

Safu Uk. 5


# Pambazuko

Toleo Namba 176 | Jumatatu, Agosti 3-9, 2026


# Wingu zito dawa za kuongeza makalio, matiti



- Serikali yaonya wanaozitangaza, kuuza

Uk. 6&7

## Mapendekezo 10 ya THRDC Katiba Mpya

Habari Uk. 22

Tafakuri ya Bagonza

## Sikiliza kisichosemwa kuliko kinachosemwa

Safu Uk. 10

## Mchakato wa maridhiano isiwe hadithi, uharakishwe

Tahariri Uk. 2

# Uchumi unapaa, mifuko ya wananchi hoi



Uk. 12

## Bandari ya Mtwara injini mpya kukuza ajira, biashara SADC

Habari Uk. 16



## Wataalamu waonya tishio ongezeko la Ukimwi

Uk. 20

## Tahariri

# Mchakato wa maridhiano isiwe hadithi, uharakishwe

GAZETI hili limewahi kuandika tahariri kuhimiza uhitaji mkubwa wa busara, uvumilivu na utashi wa uongozi unaosimamiwa na ukomavu wa historia yetu ili kuhakikisha maridhiano yanapatikana.

Katika muktadha huu, ni jambo la muhimu kuhimiza haraka mchakato wa maridhiano kati ya vyama vyetu, taasisi na umma ili kuondoa kabisa dalili za uhasama zinazoonekana kukua siku hadi siku.

Uhasama huo hauumizi tu mazingira ya kisiasa, bali pia unaathiri maendeleo ya kiuchumi, amani ya jamii na kuaminiana kwa baadhi ya taasisi za serikali kwa umma.

Ieleweke kuwa vyama vyote vinapaswa kuweka kipaumbele mazungumzo ya wazi na ya kujenga, siyo yale ya kushinikiza hasira wala kuendeleza aibu.

Maridhiano yenye maana yanahitaji kujenga msingi wa kuzungumza bila masharti magumu, kutambua makosa yaliyopita, na kujenga mikakati ya pamoja ya kuzuia migogoro inayoweza kutokea siku zijazo.

Hii inamaanisha pia kutangaza ahadi za uwazi katika mchakato wa mazungumzo, ili wananchi waone ni kwa jinsi gani mabadiliko hayo yanavyoenda kutekelezwa na kuwa na fursa ya kuyafuatilia kwa uwazi.

Taasisi za umma ikiwamo vyombo vya kutenda na kutekeleza haki, sheria na mashirika ya kiraia zinapaswa kusaidia kutuliza hali kwa kuhimiza ushirikiano badala ya kugawanya na kuhimiza kufanya kazi kwa haki na kutenda inavyotakiwa.

Nasi vyombo vya habari tuna jukumu kubwa la kuleta taarifa sahihi, kuepuka uandishi wa chuki na kuchochea uhalali wa kila habari inayofika kwa umma kuwa yenye manufaa, hata kama ikiwa ni kuikosoa serikali na viongozi wake.

Vyombo vya sheria vinapaswa kutumika kama dhamana ya uamuzi wa haki pale migogoro inapotokea, bila kujali msimamo wa kisiasa wa pande husika.

Viongozi wa vyama wanahitaji kuonyesha uongozi wa uthubutu, kwa maneno na vitendo. Lugha ya kuchochea na vitendo vya kuzuia mazungumzo vinapaswa kuepukika kwa sasa.

Viongozi wetu wanastahili kuonyesha mfano wa kuomba msamaha pale makosa yemetendeka, na kuonesha utayari kwa mashauriano ya kusamehe pale walipoumizwa na kueleza wazi nao waliumiza wapi na kwa kina nani.

Wananchi nao wanapaswa kushirikishwa katika mchakato wa maridhiano, kwani yanapowashirikisha, hujengwa jamii yenye kuaminiana na kupendana. Hii itasaidia kurejesha Tanzania iliyozoeleka machoni pa dunia.

Kushirikisha umma kutaimarisha umiliki wa mchakato na kuhakikisha kuwa suluhisho litakalopatikana inaendana na matarajio ya wengi.

Pambazuko tunahimiza kuwa ni lazima kila Mtanzania akumbuke kuwa amani ya kudumu na maendeleo yanakaribishwa zaidi kwa njia jumuishi, na siyo kufanya uamuzi wa wachache gizani.

Kuharakisha maridhiano na kuondoa dalili za uhasama kati ya vyama, umma na taasisi ni hatua muhimu mno kwa sasa ili kukomaza utaifa wetu na kurejesha staha kwa kila Mtanzania kutemba kifua mbele.

Sasa ni wakati wa kuweka maslahi ya taifa mbele, kurejesha imani kati ya wanasiasa na wananchi; watendaji na taasisi za umma na wananchi na kuunda mazingira ya utulivu yatakayowezesha Tanzania kukua kwa ustawi na maendeleo.

# Uzinduzi wa Hospitali ya Nyerere



*Rais Samia Suluhu Hassan na Rais wa Angola, João Manuel Gonçalves Lourenço wakikata utepe kuzindua Hospitali Kuu ya Rufaa ya Rais Julius Nyerere iliyopo Kilamba, jijini Luanda, Angola juzi. Hospitali imepewa jina hilo kwa heshima ya kutambua mchango wa Rais wa Kwanza wa Tanzania kufanikisha harakati za ukombozi wa Bara la Afrika, hususan nchi za Kusini mwa Afrika . Kulia ni Mama Maria Nyerere. (Picha na Ikulu).*

## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**


## TIMU YA PAMBAZUKO

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Mhariri Mkuu** | : | Simon **MKINA** | (simon@pambazuko.or.tz) |
| **Mhariri Mtendaji** | : | Peter **NYANJE** | 0784 211 716 |
| **Mwandishi Mkuu** | : | Elizabeth **HOMBO** | 0712 792 216 |
| **Mwandishi Mwandamizi** | : | Andrew **MSECHU** | 0769 415 815 |
| **Mkuu wa DTP** | : | Yassin **LUPATU** | 0782 009 971 |
| **Mkuu wa Utawala** | : | Tryruckia **MFINANGA** | 0744 768 263 |

*Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz*

# Dunia: Hapa na Pale

## Ahueni waume wagumba

WANAUME waliogunduliwa kuwa wagumba kabisa sasa wanapata tumaini baada ya wanasayansi kufanikiwa kutengeneza seli za awali za mbegu za uzazi za kiume katika maabara.

Matokeo ya utafiti huo, uliochapishwa katika jarida la kisayansi la Cell Stem Cell na watafiti wa Chuo Kikuu cha Pennsylvania, Marekani, unaonyesha hatua kubwa katika juhudi za kutengeneza mbegu za uzazi nje ya mwili wa binadamu.

Ingawa mbegu hizo hazikufikia ukomavu kamili wa kurutubisha yai, watafiti wanasema wamefikia hatua ambayo haijawahi kufikiwa katika tafiti za binadamu.

## AI yahadaa Wamarekani

WIZARA ya Mambo ya Nje ya Marekani, imewashtua wajumbe wa mkutano maalumu wa masuala ya Ukimwi nchini Brazil, baada ya kukosea ramani ya nchi za Afrika katika wasilisho lake.

Katika mkutano huo, ramani iliyowasilishwa na serikali ya Marekani iliibua mjadala, baada ya kuonyesha kuwa Nigeria, nchi ambayo Marekani tayari ina vikosi vya jeshi lake huko.

Ramani hiyo ilionyesha kuwa Nigeria iko katikati ya Jangwa la Sahara badala ya magahribi mwa Afrika, Msumbiji ikiwa katika pembe ya Afrika badala ya eneo la kusini mashariki mwa Afrika, huku Ivory Coast ikiwa katika eneo ilipotakiwa kuwepo Msumbiji badala ya magharibi mwa Afrika.



Ilibainika kuwa wasilisho hilo lililozua mkanganyiko katika mkutano huo uliokuwa ukiainisha makubaliano mapya katika sekta ya afya, huenda iliandaliwa na wataalamu ambao hata hawajui vyema Afrika na nchi zilizomo, bali walitumia akili unde (AI) ambayo iliwadanganya, nao wakaibeba hivyohivyo hadi mkutanoni.

## Utata alipo Rais Paul Biya

WANANCHI wa Cameroon hawajui iwapo rais wao, Paul Biya. Hawajui kama yu hai au ameshakufa! Hii ni baada ya kutokuwepo kwa taarifa rasmi kuhusu mahali alipo kwa zaidi ya siku 53.

Biya (93) kwa sasa ndiye rais mwenye umri mkubwa zaidi duniani, na hajaonekana hadharani wala kusikika popote, tangu ilipoelezwa kuwa amekwenda kwenye “mapumziko binafsi” nchini Uswisi Juni 7 mwaka huu.

Aliingia madarakani mwaka 1982, baada ya kuhudumu kwa miaka saba kama waziri mkuu, na kwa sasa amekuwa haonekani kwa muda mrefu nchini kwake, ikielezwa kuwa amekuwa akitumia muda huo kuongoza nchi akiwa kwenye hoteli ya kifahari ya nyota tano ya InterContinental mjini Geneva.



Waziri wake wa mawasiliano, Rene Sadi aliueleza umma kuwa ripoti zinazosambaa kuhusu afya yake kutokuwa nzuri ni uzushi kwa

## Hamas walivyosalimu amri

KUNDI la Hamas limekubali mpango uliotangazwa na Rais Donald Trump wa Marekani, kuhusu kumaliza vita vya Gaza, unaohusisha kundi hilo kusalimisha silaha zake kwa kamati ya utawala wa Wapalestina.

Mjumbe wa timu ya mazungumzo ya Hamas, Ghazi Hamad, amesema kundi hilo limekubali kufanya hatua hiyo kwa manufaa ya wananchi wa Gaza ili kuwaepusha na mauaji na kuendelea kuhama makazi yao.

Mpango huo unahusisha kuondolewa kwa hatua kwa hatua majeshi ya Israel kutoka eneo hilo. Hata hivyo, Israel haijatoa tamko rasmi kuhusu mpango huo.

Na Mzee TAI

# Wajipange, Nchimbi hana uzito wa unyoya kwenye siasa

BAADA ya kauli ya Dkt. Emmanuel Nchimbi kuhimiza Watanzania "wapambane" na "wakomae" kupata Katiba Mpya, baadhi ya watu wakaanza kukohoa kisiasa.

Wengine wakapiga chafya, baadhi waenda mwayo, wapo pia waliokimbia kutafuta kipimajoto, na wachambuzi wakaanza kupima kila neno kana kwamba limetoka kwenye mtambo wa siri.

Baadaye kidogo, nikapata taarifa kwamba mawimbi ya sauti yake yametikisa pakubwa. Siyo kwa sababu amesema Katiba Mpya ni muhimu; hilo limo katika ahadi za CCM. Kilichowasha taa nyekundu ni msamiati wa "pambaneni" na "komaeni".

Maneno hayo yamesikika kama yameazimwa kwenye mkoba wa mwanaharakati, siyo jalada la kiongozi namba mbili wa serikali.

Wapo wanaouliza; Watanzania wapambane dhidi ya nani? Wakomae kwa nani? Kama serikali inaitaka Katiba Mpya, kwa nini wananchi waambiwe waipiganie kana kwamba imefichwa chini ya godoro la mtu?

Maswali hayo yana haki ya kuulizwa, na katika siasa mambo siriazi yasipohojiwa, hugeuka mahubiri, na wananchi siyo waumini wa kukubali kila "amina" bila kujua sadaka inakwenda wapi.

Lakini wanaodhani mawimbi haya yatambeba Nchimbi kama karatasi kwenye mfereji, kwamba watamtikisa zaidi, wajipime. Huyu siyo mwanasiasa wa uzito wa unyoya.

Huyu kwa sasa ni galasa, amepita mawimbi mengi na makubwa yaliyoweza kumuimarisha na kumpa ujasiri wa kusema anachoamini. Amepita ngazi moja hadi nyingine, siyo kwa kushikwa mkono, bali haiba yake, uwezo, weledi na ukomavu wa imani yake.

Nchimbi anaijua CCM kwa korido, sebule na jiko lake. Anajua wapi chai inachemka na wapi vikombe vinagongana. Amehudumu serikalini, nje ya nchi na ndani ya chama.

Ieleweke kuwa anapotamka sentensi inayowafanya wanaharakati watabasamu, wapinzani washangae na baadhi ya wanaCCM wakune vichwa, siyo busara kukimbilia kusema ameteleza. Huenda ametembea hasa mahali anapotaka.

Hilo halimaanishi kila kauli yake ibatizwe kuwa hekima, la hasha! Makamu wa Rais anapaswa kuzungumza kwa uwazi, kwa sababu ukungu unaotoka juu huwalazimisha walio chini kutembea kwa kugongana.

Akisema wananchi wapambane, anajua kuna mkwamo sasa au huko mbele ya safari, hivyo tahadhari yake inaswii mno.

Hata hivyo, tusimjengee Nchimbi ukubwa wa kufikirika, kwa kila jambo analozungumza, na itambulike kwamba uzito wa mwanasiasa haupimwi kwa vyeo pekee, bali kwa hoja, matokeo na uwezo wa kusimamia maneno yake.

Pamoja na kuwa na usikivu hafifu – kutokana na umri mkubwa, lakini nimenasa maneno machache ya wahafidhina wanaodhani Dkt. Nchimbi ni mgeni aliyepotea Ikulu. Hawa wanajidanganya. Dkt. Nchimbi ni zao la mfumo; mwanafunzi wake na sasa mmoja wa walimu wake. Ana marafiki, historia, mtandao na nafasi ya kusikika bila kuomba kipaza sauti.

Katika siasa, sauti nzito siyo ile inayopaza kelele zaidi, bali inayobadili mwelekeo wa mjadala. Dkt. Nchimbi ametamka maneno machache, lakini wiki nzima watu wanayatafuna na katika mijadala hiyo, ni kama tayari ameshinda raundi moja.

Amewafanya wanaompinga na wanaomuunga mkono wazungumzie uwanja wa kisiasa aliouchagua mwenyewe, kwa wakati wake.

Mtazamo wangu unanieleza kuwa mawimbi ya sauti yake yanaweza kuitikisa mashua, lakini siyo rahisi kumtupa baharini.

Wanaotaka kupambana naye kwa vijembe waweke hoja mezani, siyo mihemko, waelewe kuwa bahari ya siasa ina kina kirefu, na Nchimbi hana uzito wa unyoya.

# Wingu zito dawa za kuongeza makalio, matiti




Na Elizabeth HOMBO

WANAWAKE wengi wamehadaiwa kwa matangazo ya mitandaoni kuhusu dawa za kienyeji kuongeza makalio, 'hips', kuwa na matiti yaliyosimama na kujaa vyema - ndani ya muda mfupi.

Wengi walipapatika kuona na kusoma matangazo yenye kuvutia kupitia mitandao ya kijamii na kuanza safari ya kutengeneza maumbile yao – kwa kutumiwa dawa hizo, bila kung'amua mwisho wake unavyoweza kuwalaza hospitalini, kubaki na ulemavu au pengine kaburini.

Baadhi ya wanawake walioanza au kuendelea kutumia krimu zisizothibitishwa au kudungwa sindano za silikoni kwa lengo la kukuza makalio, 'hips' na kujaza matiti, sasa wanasikitika na kushaidisha msemo huu; "majuto ni mjukuu." Wanajuta baada ya kupata madhara.

Hawa wamepata madhara ya afya zao; baadhi wakioza tishu, kuziba mishipa ya damu kuelekea kwenye mapafu, figo kushindwa kufanya kazi vyema na zaidi sana kukumbwa na changamoto za moyo na ubongo.

Pambazuko limefuatilia matangazo hayo mitandaoni, kufuatilia wauzaji, vituo vinavyotoa huduma hizo kwa siri kubwa na kuzungumza na baadhi ya wanawake wanaoishi na maumivu baada ya kutafuta maumbile yanayosifiwa mitandaoni kwa lengo la kupendeza na zaidi sana madai ya "kuvuta wanaume."

Mitandao inayoongoza kwa matangazo ya dawa hizo ni pamoja na Instagram, Tiktok, Facebook na X - zamani Twitter.

Baadhi ya matangazo hayo yanarushwa kwenye mitandao maarufu zaidi ya kijamii kupitia anwani hizi; Ungujo Cosmetics, XXL, 101 Cosmetics, Pendeza, Ng'aring'ari Shop na mengine mengi. Wanaorusha matangazo haya wakiwa wameweka nambari zao za simu wanaeleza wazi kuwa dawa zao zinaongeza makalio na kutengeneza umbo la mwanamke, ikiwamo "kuboresha matiti."

### Dini zakataza dawa hizo

Viongozi wa dini wameliambia Pambazuko kwamba kuongeza makalio au matiti, kwa maana ya kupata urembo, ni dhambi na inakatazwa na Vitabu Vitakatifu; Biblia na Quran.

Mwenyekiti wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Baraza la Waislamu Tanzania (Bakwata) na Msemaji wa Mufti, Sheikh Khamis Mataka amesema kuwa kuongeza makalio, 'hips' na matiti kwa lengo la kujipamba huangaliwa kuwa haramu kwa sababu ya kuangukia kwenye kanuni ya kubadilisha uumbaji wa Mungu.

Anasema Quran kwenye Sura ya 4, (Surat An-Nisaai), Aya ya 119 inasema kuwa; "Na hakika nitawapoteza na nitawatia matamanio, na nitawaamrisha, basi watakata masikio ya wanyama, na nitawaamrisha, basi watabadili aliyoumba Mwenyezi Mungu.

Na mwenye kumfanya Shet'ani kuwa ni mlinzi wake badala ya Mwenyezi Mungu, basi huyo amekhasiri khasara ya dhaahiri." (Qur'an 4:119).

Inaendelea Uk. 7

# Wingu zito dawa...

Inatoka Uk. 6

Mwanazuoni huyo wa Kiislamu anasema kuwa hadithi huonyesha uadui dhidi ya vitendo vya kubadilisha kwa lengo la kupotosha muonekano na kufurusha sura halisi.

Mchungaji wa Kanisa la International Biblical Pentecost (IBP) lililoko Kitunda, Dar es Salaam, Sylvester Mkude anasema kuwa ni dhambi na chukizo kwa Mungu kwa wote wanaobadili maumbile yao kwa lengo la kuvutia na siyo tiba.

Anasema pamoja na kuwa Biblia haina mistari inayokataza kukuza maumbile ya mwili moja kwa moja, lakini Mungu hapendi kurekebishwa pale alipotengeneza yeye.

Mchungaji huyo anasema Mstari wa Biblia; 1 Wakorintho 6:19–20 unaeleza kuwa mwili ni hekalu la Roho Mtakatifu; mwanadamu anapaswa kumtukuza Mungu kwa mwili wake; hivyo kuubadili kwa lengo baya, ni dhambi.

### Sheria yazifurusha dawa

Pamoja na kushamiri kwa matangazo hayo ya kukuza makalio na matiti, sheria za Tanzania zinakataza ushawishi wa uongo.

Kifungu cha 96 cha Sheria ya Dawa na Vifaa Tiba, Sura ya 219 (The Tanzania Medicines and Medical Devices Act, Cap.R.E. 2023), hukataza matangazo ya uongo na yanayopotosha kuhusu dawa na vifaa tiba, lakini bado Watanzania wameendelea kutapeliwa mitandaoni, kwani imethibitika watumiaji wapo.

Kifungu hicho cha 96 cha sheria hiyo kinakataza matangazo ya uongo au yanayopotosha kuhusu bidhaa zinazodhibitiwa na kinaweka masharti kuhusu matangazo ya dawa zinazotolewa kwa agizo la daktari. Kifungu cha 6(1) (I) cha sheria hiyo kinaipa Baraza la Tiba Asili mamlaka ya kusimamia utoaji wa taarifa na matangazo yote yanayohusu tiba asili na tiba mbadala. Lakini pamoja na sheria hizo za kudhibiti, hakuna hatua zilizochukuliwa kudhibiti matangazo mengi mitandaoni na mitaani, ambayo yanaonekana bayana kuwa ni ya kupotosha.

Kwa kiasi kikubwa Watanzania wengi hurubunika kupitia matangazo hayo na kupoteza fedha kununua dawa hizo ambazo haziwaletei matokeo yanayotarajiwa.



### Aina za dawa, vipimo

Changamoto kubwa inayoonekana kwa wanaotangaza dawa hizo ni kukosekana kwa vipimo rasmi huku baadhi ya watangazaji wakitoa ahadi na ushuhuda wa uongo kuwa dawa zinaponya kila kitu.

Kipimo kikubwa kwa dawa za maji ni kuchanganya kwenye maji ya uvuguvugu na kunywa kikombe kimoja cha chai; kila asubuhi kabla ya kula chochote na jioni, kabla ya kula chakula cha usiku.

Kwa zile dawa za krimu- za kupaka, mtumiaji anashauriwa kupaka eneo la makalio mara tatu kwa siku; asubuhi, mchana na jioni.

Pambazuko limeona moja ya hiyo krimu inayoitwa 'Big Butt' inayoaminika kutoka China, ambayo inatajwa na watengenezaji kuwa "ni kiboko kukuza makalio haraka, ikiwa na maandishi ya Kichina, ambayo yalitafsiriwa na mmoja wa watu wanaojua lugha hiyo kwa gazeti hili."

Dawa nyingine ni ile ya vidonge inayoitwa Moco Root ambayo inatajwa kuwa na virutubisho vya asili ikiaminika kuengenezwa Indonesia. Hii matumizi yake yanaelezwa kuwa ni vidonge viwili; kwa sikumara tatu.

Ipo dawa nyingine yenye jina linaloendana na hilo, ila yenyewe ikiitwa Maca Root – inatengenezwa Peru, ambayo hutangazwa kuongeza hamu ya tendo la ndoa, nayo wauzaji wanadai inakuza makalio.

Nyingine ni dawa ya maji inayoitwa Cloxino, ambayo inaonekana kutokea China ikiwa na maelezo yaliyoandikwa kwa Kichina yanayotafsiriwa kueleza kuwa yanabeba vichocheo vya homoni nyingi "salama" kukuza makalio.

Inaendelea Uk. 8

# Wingu zito dawa...

Inatoka Uk. 7

Dawa nyingine ni ile inayoitwa Volcano, ambayo iko kwenye vidonge ambayo imebainika kuwa huingizwa sehemu ya haja kubwa na kubaki huko kwa saa nne, ikitumika mara moja kwa siku. Dozi yake ni mwezi mzima, vidonge. Kila kidonge kikitumika kinaondolewa na kushauriwa kukitupa.

**Ushawishi wa kuvutia**

Mvuto wa matangazo hayo yanayoweka picha za wanawake wenye makalio makubwa, 'hips' na matiti yaliyosimama na kujaa, yanatajwa kuwa moja ya "sumaku" kuvuta wateja.

Baadhi ya watumiaji wanaeleza kuvutwa na matangazo hayo na kuamua kujaribu, hata hivyo, wengine wamekiri kusukumwa na marafiki ili kutumia dawa hizo.

Ester Damas, mkazi wa Goba jijini Dar es Salaam, aliyeajiriwa kuuza duka la vipodozi eneo la Mwenge, anasema amefilisika kwa sababu ya kutumia dawa hizo baada ya kuvutwa na matangazo mitandaoni.

Ingawa hakuwa tayari kutaja alipenda zaidi kuongeza eneo la mwili wake, anasema alihangaika kununua dawa hizo tangu mwaka 2023, ambapo alikutana na matangazo tofauti mitandaoni lakini hakupata matokeo anayopenda.

Huku akitaja majina ya wanaojitangaza kuwa na dawa za kuongeza makalio na "kutengeneza maumbile, Ester anasema mbali na dawa hizo, watangazaji hao pia huuza tiba lishe huku wakiaminisha wateja wao kuwa zinaponya.

"Nilihangaika sana kupata namna ya kubadili umbo langu, kwani sikuwa nalipenda sana, na ndipo nilivutika kwa picha za wasichana wenye maumbile mazuri nilizoziona kwenye matangazo hayo, nikiamini nami nitapata umbile zuri..."

"Lakini nimekuja kugundua ni matapeli kwa sababu nilitumia dawa za watu tofauti kama nne lakini sijapona hadi leo.

"Nikipiga mahesabu (usahihi; hesabu) pesa nilizotumia kununua hizo dawa za mitandaoni zinaweza kununua kiwanja cha maana, lakini nimejifunza hawa watu ni matapeli, serikali ifanye namna ya kuwachukulia hatua," amesema mwanamama huyo wakati akizungumza na Pambazuko.

Pambazuko lilifanya ufuatiliaji wake mitandaoni kwa takribani miezi miwili na kubaini baadhi ya wachangiaji kwenye kurasa za kampuni zinazouza dawa hizo wamekuwa wakiwatahadharisha wengine wasinunue kwa kuwa hazileti matokeo yanayoelezwa.

**Bei zake zatisha**

Gazeti la Pambazuko liliwatafuta wahusika wanaouza dawa hizo kwa kupiga simu wanazotangaza mitandaoni, lilihakikishiwa kuwa dawa hizo zina matokeo chanya na kwamba mhusika akizitumia inavyoelekezwa, anapata umbile analotaka.

Pambazuko limebaini kuwa bei za dawa hizo inatofautiana kulingana na ubora wa kifungashio chake, hasa zile za vidonge na krimu.

Zenye vifungashio vinavyovutia huuzwa kuanzia Shilingi 80,000 hadi 250,000 huku zile za vidonge zikiuzwa kwa bei ya chini; kuanzia Shilingi 45,000 hadi 150,000.

Hata hivyo, zile dawa za sindano, zenye Silikoni kuuzwa - kwa dozi moja, inayotumiwa kwa mwezi mmoja, huanza kuuzwa kati Shilingi 800,000 hadi milioni 1.

**'Dawa' zinavyofanya kazi**

Licha ya dawa zinazodaiwa kukuza makalio kutangazwa na kuuzwa, nyingi hazina maelezo ya kisayansi yanayoeleza kwa uwazi namna zinavyofanya kazi, usalama wake au madhara ya muda mrefu.

Bidhaa hizo hupatikana katika mfumo wa krimu, vidonge na sindano, huku wauzaji wakidai zinaweza kuongeza mafuta, tishu au kuimarisha ngozi ya makalio bila kubadili sehemu nyingine za mwili.

Daktari bingwa wa magonjwa ya binadamu, Patrick Mirumbe wa Hospitali ya Sandarya iliyoko Bunju A, Dar es Salaam anasema baadhi ya krimu hupenya tabaka za ngozi na kurejesha collagen na elastin; protini zinazosaidia ngozi kuwa imara na kunyumbulika kwa uwiano.

Daktari huyo anasema kuwa hakuna ushahidi thabiti kwamba krimu zinaweza kuongeza misuli au mafuta ya makalio pekee. Mara nyingi zinaweza kulainisha ngozi na kuifanya ionekane yenye mvuto kwa muda, bila kubadili ukubwa wa makalio.

Inaendelea Uk. 9

# Wingu zito dawa...

Inatoka Uk. 8

Anasema kuwa vidonge vingine hutangazwa kuwa na phytoestrogen; kemikali za mimea zinazoweza kuathiri homoni ya estrogen mwilini. Hata hivyo, watengenezaji wa 'dawa' za kukuza maumbile, huchanganya na vitu vingine "wanavyojua wao."

Phytoestrogen ni kemikali inayopatikana katika mazao ya mbegu; soya, kunde na maharage, ikiwa katika mfumo wa kemikali.

Ingawa estrogen huchangia mabadiliko ya maumbile ya kike, athari za phytoestrogen hutegemea aina, kiwango na mwili wa mtumiaji.

Anathibitisha kuwa hakuna uthibitisho wa kutosha kwamba vidonge hivyo hukuza makalio kwa usalama.

Anaeleza kuwa hatari kubwa zaidi ipo kwenye sindano za silikoni au vijazaji vingine visivyoidhinishwa.

Silikoni inaweza kusababisha mwili kuunda uvimbe na tishu ngumu kuizunguka, hali inayoweza kufanya sehemu iliyochomwa ionekane kubwa.

"Huo siyo ukuaji wa kawaida wa misuli, bali mmenyuko wa mwili dhidi ya kitu kigeni kinachoingia na kuvuruga ukawaida wake," anaongeza mtaalamu huyo wa tiba na afya.

Akielezea namna Silikoni inavyoweza kuathiri mtumiaji mwenye ndoto za kukuza maumbile yake, anasema kuwa kiambato hicho kinaweza kuhama, kuziba mishipa ya damu na kusababisha maambukizi, maumivu ya muda mrefu, kuharibika kwa tishu, ulemavu, kiharusi au kifo.

Daktari huyo anasema kuwa madhara yanaweza kujitokeza mara moja au baada ya miaka. Wanaotaka kubadili maumbile wanapaswa kuepuka bidhaa zisizosajiliwa na kupata ushauri wa daktari bingwa kabla ya kutumia dawa au kufanyiwa utaratibu wowote wa urembo.

### TMDA wazungumza

Pambazuko ilimtafuta Meneja wa Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA), Gaudensia Simwanza, ambaye alisema suala hilo liko chini ya Kitengo cha Tiba Asili na Tiba Mbadala Wizara ya Afya.

> **"Huo siyo ukuaji wa kawaida wa misuli, bali mmenyuko wa mwili dhidi ya kitu kigeni kinachoingia na kuvuruga ukawaida wake," anaongeza mtaalamu huyo wa tiba na afya.**

Alipoulizwa kuhusu dawa zinazotengenezwa Tanzania na zingine kuaminika kutoka China – kwa kuwa na maandishi ya Kichina, na nchi zingine iwapo zimeruhusiwa, alisisitiza watafutwe Baraza la Tiba Asili.

Gaudensia alipotumiwa baadhi ya picha za dawa hizo kutoka China kupitia simu yake ya mtandao wa WhatsApp, alisema hawazitambui na kwamba dawa lazima ziwe zimesajiliwa.

"Kupitia usajili pamoja na mambo mengine, lugha inayotumika katika kifungashio huangaliwa, lazime iwe Kiingereza au Kiswahili. Pia dawa zinapaswa kuuzwa katika maduka rasmi na siyo mitandaoni wala barabarani," ameongeza.

Kuhusu kuwepo matangazo ya dawa za kuongeza makalio na dawa lishe, Simwanza alisema hilo linaingia kwenye vipodozi hivyo iko chini ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

### TBS wajiweka kando

Ofisa Uhusiano Mwandamizi wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Neema Mtemvu, ameliambia Pambazuko kuwa shirika hilo halihusiki na kitu chochote kinachohusu dawa.

"Ni kweli food supplement (tiba lishe) tunakagua sisi, lakini tukigundua tu mtu anasema hiyo supplement yake inatibu ugonjwa fulani huwa tunaondoa hapohapo, sisi hatupitishi chochote kinachotibu kwani mambo yote ya dawa yako chini ya TMDA," amesema Neema.

### Baraza laeleza

Mfamasia na Mtendaji kutoka Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala Tanzania, ambaye pia amekuwa akishiriki katika shughuli rasmi za ukaguzi, Ndahani Msigwa, amesema wamejitahidi kudhibiti matangazo huku wakisaidiana na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa karibu.

Inaendelea Uk. 14

Tafakuri ya Bagonza



Na Dkt. Benson BAGONZA




# Sikiliza kisichosemwa kuliko kinachosemwa

KATIKA mazingira ya kutoaminiana, mtu anapoongea, jitahidi kusikiliza kisichotamkwa kuliko kinachotamkwa.

Ujuzi wa kusikiliza kisichotamkwa ni taaluma maalum. Wasiojua, wanaita umbea.

Sasa, nimebahatika kusikiliza kisichotamkwa na kubaini haya yafuatayo.

Kwamba, Katiba Mpya inayodaiwa siyo moja.

Kwamba, waliyoiahidi watawala wetu na wanayotaka kuileta, haitakiwi na wananchi.

Kwamba, wanayoitaka na kuidai wananchi, haitakiwi na watawala wetu.

Naamini kuwa kama ingekuwa moja, wasingemgeuka mjumbe wao aliyetuambia tudai Katiba Mpya.

Kwamba, waliomgeuka ndio wanazuia Katiba inayotakiwa na wananchi na kutaka kuleta wanayoitaka wao ambayo haitakiwi na wananchi.

Naona kwamba sasa tuna taifa lililokata tamaa. Mjumbe "anayeuawa" alitaka kuinua matumaini kwa kuchemsha mawe jikoni na kuwafanya watoto wenye njaa wasubiri chakula kisichoiva. Wanaompinga mjumbe tunawasubiri waje kutukatisha tamaa maana hawataki tufurahi.

Kwamba, hata kama hatukubaliani, tuheshimiane.

Hivi macho yangu yananidanganya? Kwamba, Kuna wananchi wengi wasiokuwa wanachama wa chama tawala, CCM?!

Kwamba, kuna waislamu wengi nje ya Baraza la Waislamu Tanzania (Bakwata)?!

Kwamba, kuna Waprotestanti wengi nje ya Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT)?

Kwamba, kunaweza kuwa na Wakristo wengi nje ya Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC)?

Katika yote haya, maana yangu ni; hulka ya hodhi (monopoly) ni kichaka cha uzembe, ubabe, ulevi wa madaraka, uvivu wa kufikiri, na kaburi la maridhiano.

Ni vyema tujifunze kuishi na wengine kuliko kuishi na sisi kwa sisi wenyewe. Tunajipenda mpaka tunajinyonya! Duh.

Tatizo la Mjaluo anayenyeshewa mvua, akikuomba kuingiza kichwa nyumbani kwako ili kujikinga mvua, ukikubali anaingiza mabega, mwishowe mzimamzima.

Tambua kwamba ukikosa pumzi unamwachia nyumba yote na kwenda kunyeshewa nje!

***Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.***



Na Dkt. Hellen Kijo BISIMBA

Kona ya Dkt. Bisimba

# Tunapoadhimisha Siku ya Mwanamke wa Afrika, tujenge kesho

JULAI 31 ya kila mwaka tunaadhimisha Siku ya Mwanamke wa Afrika.

Siku hii ilianzia mwaka 1962 mara baada ya kuundwa kwa Umoja wa Wanawake wa Afrika (Pan-African Women's Organisation (PAWO).

Kuanzishwa kwa umoja huo ni matokeo ya mkutano uliofanyika Dar es Salaam, kwa lengo la kuunganisha wanawake wa Afrika katika kupigania ukombozi wa Bara la Afrika, kujenga usawa, maendeleo na haki za wanawake.

Ukoloni wa kisiasa uliondolewa katika nchi zote za Afrika, lakini bado kuna ukoloni wa kifikra na ukoloni wa ndani kwa ndani zikiwemo changamoto za kidemokrasia, umaskini, kukosekana kwa fursa na hata ukatili wa kijinsia na ukatili wa aina nyingine nyingi.

Mambo yanayoendelea hapa nchini na hata nchi nyingine za Afrika kwa sasa, yanatuvuta kuwaangalia wanawake na kutafakari ukweli kuwa wanawake siyo waathirika tu wa uvunjifu wa haki za binadamu; bali wao ni mawakala muhimu wa mabadiliko.

Ukiangalia mwanamke ndiye anayebeba mzigo mkubwa wa athari za uvunjifu wa haki za binadamu.

Hofu zinapovuma kutokana na ukamatwaji holela, mauaji, kupungua kwa uhuru wa kujieleza au ukosefu wa haki, wanaobeba mzigo, mara nyingi ni wanawake.

Kwa kawaida tumekuwa tukifahamu kuwa wanawake wana nafasi ya kipekee ya kujenga na kukuza utamaduni wa amani na kuheshimu sheria kuanzia ndani ya familia.

Historia ya Tanzania inatuonyesha kiasi ambacho wanawake wamekuwa mstari wa mbele katika harakati za ukombozi na hata maendeleo.

Hali ya haki za binadamu ilivyogubikwa na vitisho, hofu na hata kupotea na kuuawa kwa watu, nchi imepigwa na ganzi kubwa na wengi wanatazama na kupata mshangao hasa kwa kuwa mwanamke ndiye aliyeshikilia usukani na maswali ni mengi kuwa kulikoni?

Wanawake waliosimama kidete wakati siku hii ya wanawake ikianzishwa miaka hiyo zaidi ya sitini nyuma walikuwa katika mazingira magumu na waliokuwa wanapambana naye ni mkoloni, aliyekuwa na nguvu kubwa na wao waliweka nia ya umoja na kwa pamoja waweze kufanya kila liwezekanalo Afrika iwe huru na iwe huru kwa kila hali. Tumeona azma yao ilifanikiwa na walishinda.

Kutetea haki za binadamu siyo kazi ya wanasheria au wanasiasa pekee, ni ya kila mtu na hasa tunapoona jinsi ambavyo waathirika wakuu ni wanawake.

Hapa inabidi wanawake tuwe vinara katika kuhakikisha hali ya haki za binadamu, inakuwa kwa manufaa ya binadamu nchini.

Wanawake tukatae kuona ukatili na damu zikimwagika mbele ya macho yetu, tukatae kuona ubaguzi, tukatae kabisa kushuhudia matumizi mabaya ya madaraka ambayo kwa sasa yanaonekana kama jambo la kawaida.

Mabadiliko chanya katika nchi yataweza kupatikana pale wanawake kwa umoja wetu tutakaposhiriki kikamilifu katika kupaza sauti kufuatia maamuzi ya kijamii na hata kisiasa.

Wanawake tuzungumze kwa ujasiri katika kuhakikisha heshima ya binadamu inahuishwa.

Tunapoiadhimisha siku hii ya wanawake wa Afrika mwaka huu wa 2026 tujihoji.

Hivi tunaridhika kuwakumbuka waanzilishi ambao ni wanawake wa jana au tutakuwa tayari kuwa sehemu ya wanawake wa leo wanaosimama kutetea haki za binadamu, utu wa binadamu na utawala wa sheria kwa nafasi yoyote tuliyo nayo?

Mwanamke wa Afrika inuka popote ulipo angalia hata maandiko ya vitabu vya dini yanasema, nami napenda kunukuu, 'Fungua kinywa chako kwa ajili ya bubu, utetee haki ya wote walioachwa' Mithali 31:8.

***Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.***

■ Habari

# Uchumi unapaa, mifuko ya wananchi hoi




*Gavana wa BoT, Emannuel Tutuba*

Na Mwandishi WETU

NI saa 12:30 alfajiri katika soko la Kariakoo, kitovu cha biashara jijini Dar es Salaam, Juma Mfaume, anafungua duka lake la vifaa vya ujenzi lenye ukubwa wa futi 10 kwa 12.

Mlio wa mlango wake unaungana na sauti za milango ya maduka mengine yanayofunguliwa wakati huo, wakianza safari ndefu ya kuwasubiri wateja ambao idadi yao inapungua siku baada ya siku.

Juma anasubiri wateja, lakini hawafiki kununua kama anavyotarajia. Wateja ni wachache na wengi wakifika wanauliza bei na kuomba punguzo, wakidai – "maisha magumu, hakuna pesa."

Hii ndio changamoto ambayo wafanyabiashara wengi wa Kariakoo na maeneo mengine nchini wanakabiliana nayo; maghala yaliyojaa bidhaa, lakini wateja hawapo.

Mfaume anafungua droo ya meza yake ya mbao, anatoa daftari lake la hesabu lililochakaa baada ya kutumika kwa muda mrefu, kisha anapitia kurasa zinazoonyesha miaka mitatu ya faida zinazozidi kuyeyuka.

Miaka miwili iliyopita, alinunua boksi la misumari ya mabati ya milimita 50 kwa Shilingi 45,000, lakini leo, bei ya boksi hilo hilo inafika Shilingi 62,000.

Ili apate faida ndogo tu, analazimika kuliuza kwa Shilingi 70,000, hata hivyo wateja wake wa kawaida - wakandarasi wadogo wanaojenga nyumba za makazi - huondoka mara tu wanaposikia bei hiyo.

"Wananiuliza kama ninatania," anasema Mfaume huku akifuta vumbi kwenye mabomba ya PVC yaliyoagizwa kutoka nje, ambayo yamekaa dukani bila kununuliwa kwa miezi miwili.

"Kisha wanaenda pembezoni mwa soko kununua vifaa vya bei nafuu, lakini visivyo na ubora," analalamika Mfaume, akiungana na kilio cha wafanyabiashara wengi ambao wameathirika na uwepo wa bidhaa bandia na zisizo na ubora, zinazouzwa kwa bei ya chini.

**Utofauti wa hali halisi**

Lakini takribani kilomita nane kutoka hapo Kariakoo, ndani ya kumbi za mikutano zenye viyoyozi, kuna simulizi tofauti kabisa kupitia wasilisho la mtaalamu wa uchumi.

Ripoti ya hivi karibuni ya Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) inaonyesha kuwa Pato la Taifa (GDP) linakua kwa karibu asilimia 6.0, mfumuko wa bei za bidhaa na huduma za matumizi umedhibitiwa katika wastani wa asilimia 3.3, huku nakisi ya urari wa biashara ikishuka hadi kiwango cha chini zaidi katika kipindi cha miaka mitano.

Kwa ufupi, takwimu hizi zinasema kuwa uchumi wa Tanzania unakua kwa kasi ya kuridhisha, lakini ukirudi kwa Mfaume na wenzake na kuwaleza hilo, watakushangaa kwa sababu ukuaji huo wa uchumi hauonekani mifukoni mwao au kwenye akaunti zao za benki.

**Uchumi wa kati wa chini**

Kwa mtazamo wa takwimu, injini ya uchumi wa taifa inaonekana kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa.

Tanzania imeimarisha hadhi yake kama nchi ya kipato cha chini cha kati (Lower-Middle Income Country), ikiwa na Pato la Taifa la jumla linalokadiriwa kufikia dola za Marekani bilioni 79.

Inaendelea Uk. 13

# Uchumi unapaa,

Inatoka Uk. 12

Takwimu zinaonyesha pia kuwa akiba ya fedha za kigeni inatosheleza kugharamia karibu miezi mitano ya uagizaji bidhaa kutoka nje, huku mikopo kwa sekta binafsi ikiongezeka kwa zaidi ya asilimia 20.

Lakini ukitoka ndani ya jengo la Benki Kuu zinakopatikana takwimu hizo na kuingia katika duka la Mfaume, unakutana na uhalisia ambao unatofautiana sana na takwimu hizo.

Hapa unaweza kubaki na swali ambalo hata wachumi wanaweza kupata shida kulijibu; inawezekanaje taifa lionyeshe viwango vya ukuaji vinavyovutia duniani kwenye takwimu, ilhali wananchi wa kawaida na wafanyabiashara wadogo wanaendelea kupambana ili kuhimili gharama za maisha na biashara?

Lakini jibu la swali hili lipo katika muundo wa ukuaji huo wa uchumi.

**Ukuaji unaotegemea mitaji mikubwa**

Hali hii ya kusigana kwa takwimu zinazoonyesha uchumi unakua na maisha duni ya watu wa kawaida itatokana na sababu nyingi.

Moja ya sababu hizo ni kuwa sehemu kubwa ya ongezeko la Pato la Taifa halitokani na viwanda vinavyozalisha ajira kwa wingi wala mageuzi ya kilimo kinachohusisha wananchi wengi - sekta ambazo huingiza fedha moja kwa moja katika mifuko ya wananchi.

Badala yake, ukuaji huo umejengwa zaidi kwenye uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya umma, uchimbaji wa madini kwa kiwango kikubwa na shughuli za kifedha zinazohitaji mtaji mkubwa.

Miradi mikubwa kama upanuzi wa bandari, ujenzi wa reli ya kisasa (Standard Gauge Railway – SGR) na mabwawa makubwa ya kuzalisha umeme, huongeza kwa kiasi kikubwa thamani ya uzalishaji katika takwimu za uchumi.

Miradi hiyo huwezesha mamilioni ya dola kupita katika akaunti za wakandarasi wa kimataifa na kuongeza thamani ya uwekezaji unaorekodiwa rasmi.

Hata hivyo, baada ya zege la miradi hii kukauka na mitambo mizito kusimama kufanya kazi, miradi hiyo huacha nafasi chache za ajira za kudumu kwa



Watanzania ikilinganishwa na idadi kubwa ya watu wenye umri wa kufanya kazi wanaoingia kwenye soko la ajira kila mwaka.

"Wakati muungano wa wawekezaji wa kigeni unapotumia dola milioni 500 kujenga reli, takwimu za kitaifa huonyesha ongezeko kubwa la uwekezaji wa mitaji," anasema mchambuzi wa uchumi aliyeko Dar es Salaam ambaye aliomba jina lake lisitajwe.

"Ni uzalishaji halisi, hilo halina ubishi, lakini ni kiasi gani cha hizo dola milioni 500 kinachogeuka kuwa mzunguko wa fedha katika maisha ya kila siku ya wafanyabiashara wa soko la Kariakoo? Ni kidogo sana…"

"Mitambo inaagizwa kutoka nje, gharama za uhandisi wa kiwango cha juu hutoka nje ya nchi, na wafanyakazi wa ndani hupokea mishahara ya kawaida ya kila siku ambayo mara moja hutumika kununua mahitaji yanayopanda bei kama unga wa mahindi na mafuta ya kupikia."

Matokeo yake ni uchumi wenye sura mbili tofauti; upande mmoja kuna sekta kubwa ya serikali na kampuni kubwa zenye uwezo mkubwa wa kifedha na kuzalisha takwimu zinazovutia za ukuaji, huku chini yake kukiwa na uchumi wa wananchi wa kawaida usio na mitaji ya kutosha, ambako mamilioni ya wajasiriamali wadogo wanahangaika kugawana soko dogo la matumizi ya wananchi linalozidi kubanwa.

Inaendelea Uk. 19

## Habari Kuu




# Wingu zito dawa...

Inatoka Uk. 9

"Lakini kwa kiasi kikubwa tumefanikiwa kwenye vyombo vya habari, kinachosumbua sana ni mitandao ya kijamii, kuyamaliza ni ngumu sana maana kila siku wanaibuka," amesema.

Akizungumzia kuhusu dawa za asili za kutoka nje ya nchi, amesema dawa nyingi zinazotoka nje ya nchi ni tiba lishe hivyo kama kuna dawa ya asili kutoka nje hiyo siyo halali.

Kuhusu iwapo dawa za kuongeza makalio, Msigwa amesema wanaouza dawa hizo wanafanya utapeli kwa sababu hazijaruhusiwa kisheria.

Msigwa amesema Watanzania watambue kuwa matapeli wameongezeka, hivyo wanapaswa kuwa makini na kujiridhisha wanapokutana na matangazo ya dawa hizo kama muuzaji amesajiliwa.

"Pia hakuna supplement zinazotibu ugonjwa hivyo tukigundua mtu anadanganya kuwa inatibu tutamchukulia hatua, tunaendelea kufanya ufuatiliaji tukimbaini yeyote anayeuza dawa hizo tutamchukua hatua za kisheria," amesema Msigwa.

**Wataalamu wanena**

Mtaalamu na mtafiti wa tiba asilia na mimea dawa kutoka Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS), Natorias Mgaya, amesema changamoto kubwa ya mitandao hivi sasa mtu yeyote anaweza kuitumia kujitangaza na kusema yeye ni mtaalam bila uthibitisho wa mamlaka husika.

Amesema ushauri wa kitabibu unatakiwa kutolewa na mtaalamu mwenye mafunzo ya kutambulika na wanaowajibika kwa mamlaka za afya.

"Kwa mfano labda ni daktari anaaswa kuwa amesajiliwa na chama chao, mfamasia, mtu wa lishe, kama ni nesi unakuta wote hawa wanakuwa na vyama vyao na wamekuwa wamepewa ruhusa..."

"Au hata kama ni mtu wa tiba asili wao wanafanya usajili wako chini ya baraza la tiba asili, hivyo hayo mafunzo mitandaoni yanatakiwa kutolewa na watu ambao tayari wamepata mafunzo kutoka mamlaka husika inayotambulika kisheria," amesema Mgaya.

Vilevile alieleza wasiwasi wake kuhusu dawa za mitishamba zinazotangazwa kuwa zinatibu magonjwa mengi tofauti, tofauti na hizo za kuongeza makalio au kuweka muonekano mzuri wa matiti.

"Unakuta anasema dawa ileile moja inatibu kisukari, shinikizo la damu, saratani, figo, uzazi, lakini kisayansi kila ugonjwa una chanzo chake na utambuzi wake matibabu yake yanakuwa ni tofauti japo kuna mwingiliano katika baadhi ya sehemu," amesema.

Mtaalamu huyo amesema kuwa kutibu magonjwa mengi kwa bidhaa moja yanahitaji ushahidi wa kisayansi, ubora, usalama na ufanisi wake.

Kuhusu uwepo wa dawa zinazoongeza makalio, Mgaya anasema hakuna ushahidi wowote wa kisayansi kuhusu dawa hizo.

"Unakuta baadhi ya dawa hizo zinazotangazwa zinaweza kuwa na viambata visivyoorodheshwa au hata dawa zinaongezwa kinyemela… hii ni hatari sana kwa sababu lazima zina madhara," amesema Mgaya.

Ameshauri wananchi kutonunua dawa hizo kwa kufuata matangazo hayo ya mitandaoni.

Inaendelea Uk. 15

# Wingu zito dawa...

Inatoka Uk. 14

Akitoa ushauri kwa serikali Mgaya amesema elimu kwa umma iongezwe ili wananchi waweze kutofautisha kati ya matangazo ya kibiashara na ushauri wa kitabibu.

Aidha, aliwataka Watanzania kutonunua dawa hizo kwa kufuata matangazo, bali wahakikishe zimesajiliwa na kushauriana na mtaalamu wa afya kabla ya kuzitumia.

Daktari Bingwa wa Upasuaji na Mkuu wa Idara ya Upasuaji, Hospitali ya Taifa Muhimbili - Mlongazila, Dkt. Eric Muhumba amesema wao hawazifahamu hizo dawa kwa sababu hawajazifanyia utafiti.

"Inaweza kuleta madhara ya muda mfupi au mrefu lakini madhara lazima yawepo. Hapa ni mamlaka kuzifanyia tafiti ili kubainisha kama kweli zinafanya kazi…"

"Lakini kilichopo huko mitandaoni ni ujanja ujanja wa watu kujipatia pesa," amesema Dkt. Muhumba.

Mtaalamu wa tiba-asili, aliyejitambulisha kwa jina la Hamud Maulid aliyeko Mwananyamala, Dar es Salaam, amesema dawa zake zinaongeza makalio bila madhara.

"Mimi nimefanya kazi hizi na wateja wangu wapo wengi, shida inakuja pale wanaotumia wanaacha kuendelea kutumia wanapoona maumbile yao yameongezeka, hapo sasa ndiyo shida," ameongeza.

Pamoja na kwamba Tanzania haina takwimu rasmi za kutokea kwa vifo vya baadhi ya watu wanaotumia bidhaa za kuongeza makalio na matiti, lakini upo ushahidi kwamba wapo wanaokumbwa na vifo baada ya kupata saratani, kuharibika kwa tishu na maungo mengine ya mwili.

### Dunia yazikataa

Dawa ama virutubisho vyote vya kuongeza maumbile ya mwili wa binadamu, hasa makalio, zinapigwa marufuku na kukatazwa na nchi nyingi duniani kutokana na madhara yake.

Bodi ya Famasia na Sumu ya Kenya (PPB) hukamata na kupiga marufuku bidhaa zote za urembo na dawa zinazotangazwa ama kubainika zinashawishi kutumika ili kuongeza maumbile.

Katika nchi za mabara ya Amerika, Ulaya na Asia, ikiwamo Marekani, Uingereza, Canada, Japan, India, na maeneo mengine, bidhaa za sindano (silikoni) au kemikali za kupaka zinazodai kuongeza makalio zimepigwa marufuku kabisa na taasisi zinazosimamia afya za binadamu.

### Kama unataka, zipo njia salama

Endapo unahitaji kukuza makalio ama kutengeneza matiti na maeneo mengine ya mwili wako, zipo njia salama ambazo mtu anaweza kutumia kufikia matamanio yake.

Njia hizo ni zile zinazoshauriwa na wataalamu wa afya ikiwa ni pamoja na mazoezi ya viungo (Squats & Glute Bridges). Hii hujenga na kukuza misuli ya makalio (glutes) kwa njia ya asili.

Pia kuna njia ya lishe ya protini ambayo ni kula vyakula kama mayai, nyama, samaki, na maharagwe ili kusaidia misuli kukua baada ya mazoezi.

Utaratibu mwingine mzuri wa kuongeza maumbile ni upasuaji salama (BBL), ambapo madaktari bingwa hufanya upasuaji kwa kuhamisha mafuta kutoka sehemu ya mwili (kama tumboni) na kuyaweka kwenye makalio. Njia hii ni ghali, lakini inapaswa kufanywa hospitalini tu.

### Wahusika watoa neno

Pamoja na wengi wanaohusika kutumia dawa hizi kuongeza makalio kufanya siri, wapo wachache ambao waliwahi kueleza wazi kwamba hakuna ukweli katika matokeo ya kutumia dawa hizo za kienyej; ziwe za kiasili kutoka Tanzania ama nje – hasa China.

Watu watano waliozungumza na Pambazuko - wote wakiwa wakazi wa Dar es Salaam, wameomba kufichwa kwa majina yao wamethibitisha madhara waliyokutana nayo kama yalivyoelezwa na wataalamu wa afya na kuchapishwa na gazeti hili.

Hata hivyo, mmoja wao, mwanamitindo wa Tanzania, maarufu kwa jina la Muna Love, amesema kuwa dawa za asili za kuongeza makalio hazifanyi kazi na wanasambaza ama kuuza, ni waongo.

Muna Love ambaye baadaye alisema aliamua kufanya upasuaji wa kitaalamu ili kutimiza ndoto yake ya kuongeza makalio na hakika alifanya, ingawa baadaye alitangaza kujuta kufanya upasuaji huo.

■ Uchumi

# Bandari ya Mtwara injini mpya kukuza ajira, biashara SADC



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), Plasduce Mbossa

**Na Mwandishi WETU**

BANDARI ya Mtwara haipaswi tena kutazamwa kama kituo cha kusafirisha korosho pekee, bali injini inayoweza kubadili uchumi wa Kusini mwa Tanzania na kuimarisha biashara ndani ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).

Ilipo kwenye Bahari ya Hindi, bandari hiyo inaweza kuwa njia fupi na yenye ushindani kwa mizigo ya Malawi, Zambia, kaskazini mwa Msumbiji na maeneo mengine ya ukanda huo.

Mabadiliko hayo yameanza kujidhihirisha na kuonekana wazi kupitia jitihada zinazosimamiwa vyema na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA).

Hadi sasa, Bandari ya Mtwara ina gati mbili zenye jumla ya urefu wa mita 685, kina cha mita 9.5 hadi 13 na eneo la hifadhi la mita za mraba 159,000.

Gati jipya lenye urefu wa mita 300 na kina cha mita 13 limeiwezesha bandari hiyo kupokea meli kubwa zaidi, huku yadi, vifaa vya kuhudumia mizigo, mifumo ya usalama na barabara unganishi vikiboreshwa. Serikali imewekeza takribani Shilingi bilioni 157.8 katika gati hilo jipya na miundombinu yake.

Matokeo yake yanaonekana katika shehena ambazo zinaendelea kupokelewa na bandari hiyo.

TPA inaeleza kuwa Bandari ya Mtwara ilihudumia zaidi ya tani milioni 2.5 katika mwaka wa fedha 2024/2025, kutoka tani 500,000 mwaka 2021/2022.

Tangu Septemba 2025, imeanza pia kupokea shehena za mafuta zinazosafirishwa kwenda Malawi na Zambia. Hii ni ishara kuwa bandari inaweza kuvuka utegemezi wa korosho na kuhudumia mafuta, makaa ya mawe, saruji, mbolea, kemikali, vifaa vya miradi, gesi na bidhaa za viwandani.

Ujio wa wafanyabiashara kutoka Comoro Aprili 2026 na mipango ya kupitisha vifaa vya mradi wa gesi kuanzia Agosti 2026 vinaonyesha kuwa masoko mapya yanafunguka. Haya ni matarajio yanayoungwa mkono na mahitaji halisi ya biashara, si ndoto ya miundombinu isiyotumika katika eneo hili.

Matarajio yanaongezwa na ujenzi wa Bandari ya Kisiwa Mgao, Mtwara, unaogharimu Shilingi bilioni 435. Mradi huo, unaotarajiwa kukamilika Julai 2028, umebuniwa kuhudumia mizigo inayotoa vumbi au uchafu, ikiwamo makaa ya mawe, saruji, kemikali na mbolea.

Kwa kutenganisha mizigo hiyo na shughuli nyingine, Kisiwa Mgao itapanua uwezo wa ukanda wa Mtwara, kuboresha usalama na kuipa bandari kuu nafasi zaidi ya kuhudumia korosho, makasha na shehena safi. Serikali pia imeelekeza kujengwa barabara ya njia nne yenye kilomita 17 kukabili ongezeko la malori.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania, Plasduce Mkeli Mbossa, ana jukumu muhimu la kuhakikisha uwekezaji huu unatafsiriwa kuwa huduma za haraka, salama na zenye gharama shindani.

Inaendelea Uk. 17

# Bandari ya Mtwara

Inatoka Uk. 16

Msisitizo wa TPA kuhusu ushirikiano kati ya bandari, wafanyabiashara, wakulima, wasafirishaji na taasisi za serikali ni wa msingi, kwa sababu gati pekee haliwezi kutengeneza biashara bila mnyororo madhubuti wa usafirishaji.

Faida kubwa zaidi itakuwa ajira, ambapo ongezeko la meli na mizigo litahitaji mabaharia, waendeshaji mitambo, wahandisi, madereva, mawakala wa meli na forodha, walinzi, wataalamu wa Tehama, bima na benki.

Nje ya lango la bandari, kutahitajika maghala, hoteli, migahawa, karakana, vituo vya mafuta, kampuni za usafirishaji na viwanda vya kuchakata mazao. Hizi ni ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja zinazoweza kuwafikia vijana na wanawake wa Tanzania na kuzalisha fursa katika nchi zinazotumia Ushoroba wa Mtwara.

Kwa wakulima wa korosho wa Mtwara, Lindi na Ruvuma, bandari yenye ufanisi inaweza kupunguza gharama na muda wa kusafirisha mazao. Hata hivyo, faida kubwa zaidi itapatikana iwapo korosho, mbaazi, ufuta na mazao mengine yatachakatwa kusini kabla ya kusafirishwa.

Badala ya kuuza malighafi pekee, Mtwara inaweza kuvutia viwanda vya mafuta, vyakula, vifungashio, mbolea na vifaa vya ujenzi, hivyo kuongeza thamani, mapato ya kodi na ajira.

Kwa nchi za SADC zisizo na bandari, hasa Malawi na Zambia, njia ya Mtwara ni mbadala unaopunguza utegemezi wa bandari chache na kuongeza ushindani wa njia za biashara.

Uwezo huo pia utaifanya Tanzania kupata mapato ya huduma za bandari, ushuru, usafirishaji na uwekezaji, huku wafanyabiashara wa ukanda wakinufaika na njia salama zaidi kuelekea masoko ya Asia na Mashariki ya Kati.

Hata hivyo, matarajio hayo hayatatimia yenyewe. Serikali lazima ikamilishe barabara, ihuishe mpango wa reli ya Kusini, iboreshe vituo vya mipakani na kupunguza urasimu.

Wafanyabiashara wanaeleza kuwa TPA inapaswa kuweka tozo shindani, mifumo mizuri ya kidijitali, ratiba zinazotabirika na ulinzi wa mazingira ili kuendelea kuimarisha uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla wake.

Haya yakifanyika vyema, wananchi wa Mtwara, na Tanzania kwa ujumla, hawatabaki kuwa watazamaji wa kusoma takwimu, bali washiriki wenye kunufaika zaidi.

Bandari ya Mtwara sasa ina miundombinu, eneo na nafasi ya kijiografia ya kutosha kuwa lango muhimu la SADC, hasa kwa kuunganishwa na reli, barabara, viwanda na diplomasia ya biashara, uwekezaji huu unaweza kugeuka kuwa mapato makubwa kwa taifa, ajira nyingi na ustawi mpana wa ukanda wa Kusini.



# TIB yanadi Dira 2050 Afrika Kusini



Deogratius Kwiyukwa

Na Benny MWAIPAJA, Durban

MKURUGENZI Mtendaji wa Benki ya Maendeleo Tanzania (TIB), Deogratius Kwiyukwa, amesema kuwa uunganishaji nguvu ya pamoja ya taasisi za kifedha katika nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), utachochea ujenzi wa viwanda vitakavyokuwa chachu ya kukuza maendeleo.

Kwiyukwa amesema hayo kando ya Mkutano wa 9 wa Wiki ya Viwanda ya SADC (SADC Industrialisation Week) unaoendelea katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa jijini Durban, Afrika Kusini. Amesema kuwa TIB ambayo ni taasisi ya serikali imeshiriki katika mkutano huo kutafuta fursa za kushirikiana na taasisi nyingine za kifedha ndani ya ukanda wa SADC ili kuunganisha mitaji kwa ajili ya kufadhili miradi mikubwa ya maendeleo itakayochangia kufikia lengo la utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 inayotaka uchumi wa Tanzania ufikie thamani ya dola za Marekani trilioni moja ifikapo mwaka huo. Kwiyukwa amesisitiza kuwa ujenzi wa viwanda vitakavyoongeza thamani ya bidhaa za kilimo, madini adimu, na bidhaa nyingine vitakavyochochea ajira na mauzo ya nje unahitaji uwekezaji mkubwa wa mitaji.

Mkurugenzi huyo amesema kuwa Tanzania imewekeza kwenye reli ya SGR, bandari, nishati, barabara na usafirishaji, hatua inayofuata ni kuhakikisha mali hizo zinazalisha shughuli za kiviwanda kuunganisha SGR, bandari, umeme na hifadhi za viwanda, kanda maalum za kiuchumi, maeneo ya madini, vituo vya kilimo na masoko ya nje.

Amesema kuwa TIB, kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Fedha za Ukanda wa SADC, inaweza kufadhili mifumo mizima ya kiuchumi inayozunguka miundombinu hiyo ya reli inayochochea viwanda kando ya njia yake, bandari inayosaidia biashara ya ghala na usafirishaji, umeme wa uhakika unaovutia viwanda vinavyotumia nishati nyingi.

Alisema kuwa mpaka sasa TIB imeviwezesha viwanda na sekta nyingine kadhaa za umma kupata mikopo nafuu kwa ajili ya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo kama vile kahawa, sukari, miradi ya maji na kwamba ikiwezeshwa zaidi kimtaji itafanya mambo makubwa zaidi.

Baadhi ya washiriki wa mkutano huo wamebainishwa kuwa wamevutiwa na fursa nyingi zinazopatikana nchini Tanzania na kuahidi kutafuta taarifa zaidi za maeneo wanayotaka kuwekeza.

Mkutano wa tisa wa Wiki ya Viwanda wa SADC umewakutanisha viongozi wa serikali, sekta binafsi, wawekezaji, taasisi za kifedha, wataalamu na wadau wa maendeleo kutoka nchi wanachama wa SADC.

Kaulimbiu ya mkutano huo ni; "Kukuza Viwanda Imara, Endelevu na Jumuishi kupitia Maendeleo ya Miundombinu, Mageuzi ya Kilimo na Madini kwa Ajili ya Dunia Yenye Haki." Kwa ujumla, mijadala ya mkutano huo imeweka msisitizo mkubwa katika kuimarisha ushirikiano wa kikanda, kuongeza thamani ya rasilimali za madini na bidhaa nyingine kabla ya kuuzwa nje, pamoja na kuhamasisha uwekezaji katika viwanda, miundombinu na miradi ya maendeleo.

# Uchumi unapaa,

Inatoka Uk. 13

**Kitendawili cha mikopo**

Kisha kuna swali la msingi kuhusu mabilioni ya fedha zinazoingia kama mikopo. Swali hapa ni kuwa fedha hizo zinaelekezwa wapi hasa? Wakati takwimu rasmi zinaonyesha kuwa mikopo kwa sekta binafsi imeongezeka kwa kasi ya asilimia 20.3, wafanyabiashara wadogo kama Mfaume na wenzake mara chache huona manufaa ya ongezeko hilo.

Kwa kuwa benki za biashara zinaweza kununua hati fungani za serikali zenye hatari ndogo na zinazotoa faida nzuri ya tarakimu mbili ili kusaidia kugharamia nakisi ya bajeti ya serikali - ambayo iko sawa na asilimia 3.4 ya Pato la Taifa – hao ndio wanufaika na ukopaji huo.

Kwa upande mwingine, msukumo wa taasisi hizo kutenga fedha kwa ajili ya mikopo ya wafanyabiashara wadogo kama Mfaume unakuwa mdogo sana kwa sababu wana fursa nyingine kubwa na ya uhakika ya kuikopesha serikali.

Hali inatarajiwa kuwa ngumu zaidi mwaka huu ambapo kupitia bajeti serikali imeshaonesha kuwa inapanga kukopa zaidi kwenye vyanzo vya fedha vya ndani baada ya vyanzo vya nje kusuasua.

Mikopo inayofika kwenye sekta binafsi mara nyingi inaelekezwa zaidi kwa kampuni kubwa zilizojijengea historia ya biashara na yenye dhamana kubwa, au hutolewa kama mikopo ya muda mfupi kwa matumizi binafsi yenye gharama kubwa za riba kwa mwaka.

"Nikienda benki kuomba mkopo wa kupanua biashara yangu, wanataka hati mbili za nyumba au ardhi, hesabu za ukaguzi za miaka mitatu, halafu wanakupa riba kati ya asilimia 18 hadi 21," anasema Mfaume huku akiegemea kaunta yake.

"Ni nani anayeweza kupata faida ya asilimia 21 akiuza misumari na saruji wakati wateja wake wenyewe wanahangaika hata kumudu mkate?"

Ili kuendelea kuishi kibiashara, wafanyabiashara wadogo wameanza kutegemea programu za mikopo midogo kwa simu au vikundi visivyo rasmi vya kukopeshana fedha.

Mifumo hii hutoa fedha kwa haraka kupitia simu, lakini kwa gharama kubwa sana za riba ambazo humeza faida ndogo wanazobakiwa nazo.

Ni kweli kwamba huu ni ushirikishwaji wa kifedha - takwimu zinaonyesha zaidi ya asilimia 76 ya watu wazima sasa wanaweza kupata huduma rasmi za kifedha - lakini kwa sehemu kubwa ni ushirikishwaji katika mzunguko wa madeni ya muda mfupi badala ya kujenga utajiri wa muda mrefu.

**Ukweli kwenye biashara**

Kufikia mchana, joto na unyevunyevu katika eneo la Kariakoo vinakuwa vikali. Mfaume ameweza kufanya mauzo mawili pekee; jozi moja ya glavu za kazi na chupa ndogo ya kimiminika cha kusafishia. Jumla ya mapato - Shilingi 14,000 (takriban dola 5.20) kwa siku.

Nje ya mlango wa duka lake, kijana aliyehitimu chuo kikuu akiwa ameshikilia jalada lenye nakala za vyeti na wasifu anapita, akiwakwepa machinga wanaouza viatu vya mitumba vilivyopangwa juu ya maturubai ya plastiki.

Takwimu rasmi zinazoonyesha ukuaji wa Pato la Taifa kwa kila mwananchi kwa kiwango cha asilimia 3.1 zinaashiria kuwa kila Mtanzania anazidi kuwa tajiri kidogo kidogo kila mwaka.

Lakini pale ambapo ongezeko la watu linaendelea kuwa kubwa na uundaji wa ajira rasmi hauendi sambamba na makumi ya maelfu ya vijana wanaoingia kwenye soko la ajira kila mwaka, takwimu hizo huwa hazitoi faraja kubwa kwa wananchi.

Simulizi kubwa la mafanikio ya uchumi wa taifa si la uongo - barabara zimepanuka, majengo marefu yanaongezeka, na kinga za uchumi kwa kiwango kikubwa zipo.

Lakini hadi pale thamani inayozalishwa na ukuaji wa juu wa uchumi itakapofika kwa wananchi kupitia kupungua kwa gharama za uzalishaji, mikopo nafuu ya biashara na ongezeko halisi la mishahara, safari ya kuelekea uchumi wa kipato cha kati itaendelea kuonekana kama simulizi la nchi mbili tofauti zinazoishi chini ya bendera moja.



■ Habari

# Wataalamu waonya tishio ongezeko la Ukimwi




Na Mwandishi WETU

NCHI za Afrika zimehimizwa kubuni miradi kwa lengo la kupambana na tishio jipya la ongezeko la maambukizi ya Ukimwi.

Ushauri huo unafuatia onyo la Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Ukimwi (Unaids), kuhusu kuwepo tishio jipya la janga la ukimwi duniani.

Hofu hiyo inatokana na kupungua kwa ufadhili wa kukabiliana na ugonjwa huo, wataalamu wa afya wamezishauri nchi za Afrika kutafuta njia za kujitegemea katika eneo hilo.

Kwa mujibu wa ripoti mpya ya Unaids iliyozinduliwa hivi karibuni huko Rio de Janeiro, Brazil, dunia imeingia katika kipindi cha kubana matumizi na kupungua kwa ufadhili wa sekta ya afya.

Hali hiyo inaweza kuathiri upatikanaji wa huduma za kinga, upimaji na matibabu ya virusi vya Ukiwmi (VVU) katika nchi nyingi, ikiwemo Tanzania.

Wataalamu wa afya wanaonya kuwa endapo pengo la ufadhili halitazibwa, baadhi ya nchi zinazotegemea misaada ya nje kugharamia huduma za kinga, upimaji na matibabu ya VVU zinaweza kushuhudia kuongezeka kwa maambukizi mapya na kudorora kwa mafanikio yaliyopatikana katika miaka ya karibuni.

Akizungumza na Pambazuko, mwanaharakati wa afya anayetoa huduma, elimu na uhamasishaji wa afya kupitia vituo vya kutolea huduma na mitandao ya kijamii, Dkt. Gaudence Mathew, amesema Afrika itabidi ijitegemee.

"Tubuni miradi yetu tuje na dawa zetu ambazo zinaweza kupambana na HIV tusitegemee tu hiyo misaada eti ndiyo kila kitu," ameshauri Dkt. Mathew.

Kwa upande mwingine, Dkt. Mathew anasema suala hilo pia linaweza lisisababishe ongezeko la maambukizi ya VVU bali litakwenda kupunguza kwa sababu watu watakuwa wanaogopa kupata Ukimwi kwa vile dawa zitakuwa hazipatikani kirahisi.

"Watu wataogopa kushiriki ngono zembe na kuepuka njia zote zile ambazo zinapekelea maambukizi, hivyo mipango yao hata ikija itaongeza umakini zaidi kwa jamii zetu,"amesema Dkt. Mathew.

**Utafiti wa Tacaids**

Takwimu za Utafiti wa Kitaifa wa Athari za Virusi vya Ukimwi Tanzania 2022/2023, uliofanywa na Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (Tacaids) kwa kushirikiana na serikali, zinaonyesha kuwa watu wazima wapatao milioni 1.55 wanaishi na VVU nchini huku kiwango cha maambukizi kikiwa asilimia 4.4.

Utafiti huo pia unaonesha kuwa Tanzania inarekodi wastani wa maambukizi mapya 60,000 ya VVU kila mwaka miongoni mwa watu wenye umri wa miaka 15 na kuendelea.

Aidha, matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa asilimia 82.7 ya watu wanaoishi na VVU wanajua hali zao, asilimia 97.9 ya wanaojua hali zao wanatumia Dawa za Kufubaza Virusi (ARV).

Inaendelea Uk. 21

# Wataalamu waonya

Inatoka Uk. 20

Asilimia 94.3 ya wanaotumia dawa hizo wakiwa wamefikia kiwango cha kudhibiti virusi mwilini, hatua inayoonyesha maendeleo katika utoaji wa huduma za matibabu na ufuatiliaji.

Akizungumza na Clouds TV wiki iliyopita, mwakilishi kutoka Tacaids, Nyangusi Laizer, alisema kwa mujibu wa utafiti huo, wanawake wanaongoza kwa maambukizi ya Ukimwi kwa asilimia 5.6 huku wanaume ni asilimia 3.

"Katika maambukizi hayo mapya asilimia 40 yanatoka kwa vijana wenye umri kuanzia miaka 15 hadi 24. Na vijana wa kike wanabeba asilimia 84 ya maambukizi," amesema Laizer.

Amesema hadi sasa mkoa wa Njombe unaongoza kwa maambukizi ya Ukimwi nchini ukiwa na asilimia 12.7 ukifuatiwa na Iringa asilimia 11.1 na Mbeya asilimia 9.6.

Ripoti mpya ya Unaids, inaonyesha kuwa ufadhili wa kimataifa wa mapambano dhidi ya Ukimwi ulipungua kwa asilimia 18 mwaka 2025 na kufikia dola bilioni 7.3, kiwango cha chini zaidi katika kipindi cha karibu miongo miwili.

Kabla ya kuingia madarakani kwa Rais wa Marekani, Donald Trump, Marekani ilikuwa mfadhili mkuu wa mapambano dhidi ya Ukimwi duniani, ikichangia takribani asilimia 75 ya ufadhili wote wa kimataifa.

Daktari bingwa wa binadamu kutoka Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) ambaye hakutaka jina lake kutajwa gazeti akisema siyo msemaji rasmi, ameliambia Pambazuko kuwa onyo hilo la Unaids, linaweza kurudisha nyuma mafanikio yaliyopatikana miaka ya karibuni katika kupambana na maambukizi ya VVU.

"Tishio hilo la Unaids, inaibua umuhimu wa kuendelea kuimarisha vyanzo vya ndani vya ufadhili wa mapambano dhidi ya VVU, ili kuhakikisha huduma za kinga, upimaji na matibabu zinaendelea kutolewa bila kutetereka hata kama misaada kutoka kwa wahisani wa kimataifa itapungua," amesema mtaalamu huyo wa afya.

Julai 27, 2026, Mkurugenzi Mtendaji wa UNAIDS, Winifred Byanyima, alinukuliwa na vyombo vya habari akisema, pamoja na mafanikio makubwa ya kisayansi yaliyopatikana katika kudhibiti VVU, kupungua kwa misaada kunahatarisha maendeleo yaliyofikiwa na kuongeza pengo la upatikanaji wa huduma za afya.

"Ripoti hii inaonyesha mambo mawili. Kwanza ni maendeleo makubwa ya kisayansi yaliyopatikana, lakini pili ni onyo kwamba kupungua kwa misaada kunazidisha ukosefu wa usawa, kunadhoofisha haki za binadamu na kuweka maisha ya mamilioni ya watu katika hatari," amesema Byanyima.



*Kamera ya Pambazuko jana ilimenasa daraja linalounganisha maeneo ya Kigogo na Msimbazi likiwa limekamilika kwa asilimia 90. Kumalizika kwa kwake kutaondoa tishio kubwa la mafuriko ambalo limekuwa likitokea mara kwa mara na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wakazi wa Dar es Salaam.*

# Mapendekezo 10 ya THRDC Katiba Mpya

**Na Mwandishi WETU**

MTANDAO wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), umetoa mapendekezo 10 ya mchakato wa Katiba Mpya, ukieleza nini cha kufanya kufufua mchakato huo hadi mwisho wake.

Akitoa mapendekezo hayo juzi, Mratibu wa THRDC, Onesmo Olengurumwa amesema pendekezo la kwanza ni uponyaji wa taifa na uwajibikaji kwa matukio ya Oktoba 29, 2025, pamoja na matukio mengine yanayohusisha utekaji.

“Ni muhimu taifa kwanza kushughulikia suala la uponyaji na maridhiano, hii inaweza kufanyika kwa kushirikisha mtu au taasisi huru yenye kuaminika ili kusaidia mchakato wa upatanisho kati ya makundi yote yaliyoathirika au kuathiriwa na matukio hayo,” amesema Olengurumwa.

Alilitaja pendekezo la pili kuwa ni serikali kuanzisha mchakato wa maridhiano ya kitaifa utakaodumu kwa kipindi cha miezi mitatu kwa kuwashirikisha makundi yote ya kijamii.

Olengurumwa amesema pendekezo la tatu ni kutungwa au kurekebishwa kwa sheria ya mabadiliko ya Katiba, kazi ambayo itafanyika kuanzia Desemba 2026 hadi Februari 2027.

Amesema baada ya kufikiwa kwa mwafaka wa kitaifa, Bunge litunge au lirekebishe Sheria ya Mabadiliko ya Katiba ili kuweka msingi wa kisheria wa mchakato mzima.

Pendekezo la nne amesema ni kuundwa kwa kamati ya kitaifa ya wataalamu kuanzia Machi mwaka 2027.

“Iundwe kamati ya kitaifa ya wataalamu yenye wajumbe wasiozidi 25 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar…”

“Kamati hiyo iwe na jukumu la kupitia na kuoanisha maudhui ya Rasimu ya Jaji Warioba, Katiba Pendekezwa ya mwaka 2014 na Katiba ya sasa kwa kuzingatia maoni ya wananchi yaliyokusanywa katika mchakato uliopita,”amesema.

Ametaja pendekezo la tano kuwa ni uandaaji wa Rasimu ya Katiba Pendekezwa kuanzia Machi – Agosti 2027.

Pendekezo la sita, amesema liundwe bunge dogo la Katiba Septemba mwaka 2027, baada ya kamati ya wataalamu kukamilisha rasimu na likae kwa muda usiozidi siku 30 kwa ajili ya kupitia, kujadili na kuboresha rasimu hiyo.

Amesema pendekeo la saba ni elimu ya Katiba Mpya na ushirikishwaji wa wananchi Oktoba 2027 hadi Januari 2028.

“Rasimu iliyoboreshwa na Bunge la Katiba itolewe kwa wananchi kwa kipindi cha miezi minne kwa ajili ya elimu ya uraia, mijadala ya umma na kupokea maoni ya mwisho,”amesema.


Mratibu huyo wa THRDC, amesema pendekezo la nane ni kura za maoni Februari hadi Machi, 2028, ambapo wananchi wataamua kuhusu Katiba Mpya kupitia kura ya maoni kwa wao ndiyo wenye mamlaka ya mwisho.

Pendekezo la tisa, ni marekebisho na uoanishaji wa sheria zote na Katiba Mpya Aprili mwaka 2028 hadi Juni 2029.

Amesema iwapo Katiba Mpya itaidhinishwa na wananchi kupitia kura ya maoni, serikali na bunge waanzishe mchakato wa kupitia, kurekebisha na kuoanisha sheria zote za nchi ili ziendane na masharti, misingi na taasisi mpya zitakazoanzishwa na Katiba Mpya.

Pendekezo la mwisho ni kutangazwa na kuanza kutumika kwa Katiba Mpya Julai mwaka 2029.

Olengurumwa alihitimisha kuwa ratiba hiyo itawezesha Tanzania kukamilisha mchakato wa Katiba Mpya kwa njia ya utaratibu unaojenga maridhiano ya kitaifa, ushirikishwaji wa wananchi na uhakika wa kisheria.



# Mwendokasi isiwe adhabu kwa maskini wa Mbagala

Na Mwandishi WETU

SAA 12 jioni, mama lishe wa Mbagala, Dar es Salaam, anafungua pochi yake na kuhesabu Shilingi 3,200 alizopata siku hiyo kwenye biashara yake.

Mwezi mmoja uliopita, fedha hizo zingeweza kumlipia nauli ya kwenda na kurudi mjini na kubakiza kiasi cha kununua mboga. Leo, sehemu kubwa ya pesa hizo inaweza kuishia njiani baada ya kulazimika kuunganisha usafiri.

Kuanzia Julai Mosi, 2026, Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ilielekeza daladala zinazotoka Mkuranga, Tuangoma na maeneo mengine ya pembezoni kuwashusha abiria katika Kituo cha Mbagala Rangi Tatu.

Hapo, abiria wanapaswa kuunganisha safari kwa mabasi yaendayo haraka kuelekea Kariakoo, Kivukoni na katikati ya jiji.

Daladala za Mbagala–Kariakoo au Kivukoni zilitakiwa kutumia vituo vilivyopangwa bila kupakia wala kushusha abiria katika ukanda wa mwendokasi.

Lengo la kulinda uwekezaji wa serikali na kuondoa mwingiliano wa huduma linaeleweka.

Ieleweke kuwa Dar es Salaam inahitaji usafiri wa umma wa haraka, salama na unaotabirika. Tatizo ni utekelezaji unaoweza kumfanya mwananchi wa kipato cha chini kuwa gharama ya kwanza ya mageuzi hayo.

Serikali inaweza kuwa sahihi kutaka uwekezaji wa mabilioni ya shilingi utoe matokeo, lakini ufanisi haujengwi kwa kuondoa ushindani kabla huduma mbadala haijawa imara.

Mfumo mzuri huwashawishi abiria kwa ubora, muda na bei; hauwalazimishi kuingia kwa sababu tu chaguo lao limefungwa. Ushindani uliodhibitiwa unaweza hata kuilazimisha BRT kuboresha huduma na kuwajibika zaidi kwa kila shilingi inayolipwa na abiria wake.

Kwa anayetoka Kongowe, Kisemvule au Mkuranga, hiyo inaongezwa juu ya nauli ya kufika Mbagala. Tofauti ya Shilingi 400 au 500 kwa siku inaweza kufikia takribani Shilingi 12,000 hadi 15,000 kwa mwezi.




Mama lishe, machinga au mlinzi anayepokea Shilingi 150,000, hiyo siyo chenji; ni chakula, dawa au sehemu ya mahitaji ya shule kwa Watoto wake.

Kinachoongeza wasiwasi ni kwamba, wakati agizo likitolewa, MOFAT ilikuwa ikiendesha mabasi 50 pekee kati ya 200 yaliyowekezwa—asilimia 25 tu.

Hoja kwamba daladala zinayafanya mabasi ya mwendokasi yakose abiria inahitaji uchambuzi mpana. Kwa nini wananchi wanachagua daladala zenye msongamano badala ya mabasi ya kisasa? Majibu yanaweza kuwa nauli, upatikanaji, urahisi wa njia na muda wa kusubiri.

Historia ya Barabara ya Morogoro inapaswa kuwa onyo kwani daladala ziliondolewa baada ya kuanza kwa awamu ya kwanza ya mwendokasi, lakini Novemba 2025 Latra ilitoa nafasi 150 za vibali vya muda kwa mabasi ya mijini kutokana na changamoto za huduma. Mbagala isirudie filamu hiyo.

Suluhisho siyo kuua mwendokasi, bali kuujenga kwa weledi na uamuzi wenye tija. Kabla ya kubana daladala, mabasi ya kutosha yawekwe barabarani; tiketi zipatikane kwa urahisi; foleni zipunguzwe; na nauli iangaliwe kwa kuzingatia uwezo wa wananchi.

Pia, njia mlishi pia zipangwe ili abiria wasilipe mara nyingi kwa safari moja.

Mwendokasi unapaswa kupunguza gharama na adha, siyo kuziongeza, vinginevyo, Mbagala haitakumbukwa kama mwanzo wa usafiri wa kisasa, bali mahali ambapo Serikali ililinda uwekezaji wake kwa kuubebesha mzigo mwananchi maskini. Chelea chelea, utamkuta mwana siyo wako.



Na Loth MAKUZA

# Kampuni zisizojifunza hatarini kuanguka

KABLA kampuni haijaanguka kibiashara, kwanza huanguka kwenye mawasiliano yake. Hilo halina ubishi duniani kote.

Kampuni zinatumia mabilioni ya fedha kwenye mabadiliko ya kidijitali, lakini imebainika kuwa asilimia 70 ya miradi hiyo inashindwa kufikia malengo yake.

Tatizo siyo teknolojia, bali ni watu na jinsi wanavyoelezwa nini kinaendelea.

International Data Corporation (IDC) wanasema matumizi ya kidijitali duniani yatavuka dola trilioni tatu mwaka huu 2026.

Fedha hizi ni nyingi, lakini matokeo hafifu, kwa nini?

Sababu zipo nyingi, lakini upo uwezekano wa timu za mawasiliano kugeuka kuwa viwanda vya kutengeneza vipeperushi.

Zinahesabu mafanikio kwa idadi ya kampeni zilizozinduliwa, siyo kwa kile kilichobadilika ndani ya kampuni.

Hii ndiyo tabia ya 'uchawa' wa kikazi. Unafanya kazi nyingi, unaonekana 'busy', lakini hujaathiri chochote. Bosi anataka kusikia kampeni tano zimezinduliwa, sio kuuliza kama wafanyakazi wameelewa kwa nini mabadiliko yanafanyika.

Ripoti ya Harvard Business Review inasema asilimia 95 ya wafanyakazi hawaelewi mkakati wa kampuni zao.

Nina wasiwasi kwamba hata pale viongozi wanapoamini wamewasiliana vizuri, idadi hiyo haibadiliki sana.

Kuwaeleza watu jambo siyo sawa na kuwawezesha kubadilika, mtu anaweza kusikia tangazo redioni asubuhi bila kubadili tabia yake mchana.

Swali la msingi siyo - 'tunahitaji kutangaza nini?' bali ni 'wapi ukimya wetu unaweza kutuua?' Hapo ndipo mchezo unapobadilika.

Badala ya kuandaa kampeni zinazofuata ratiba ya bosi, unatafuta maeneo ambayo kutoelewana au kutofautiana kunaweza kuzamisha mradi mzima.

Utafiti unaeleza kuwa kampuni zenye mfumo mzuri wa kusimamia mabadiliko zina uwezekano wa mara saba zaidi kufikia malengo yao ya mabadiliko.

Ukiingiza mawasiliano mapema kwenye mpango wa mabadiliko, siyo mwishoni kama kiungo cha ziada, unaongeza nafasi ya kufanikiwa.

Tatizo la wengi ni kupanga mawasiliano kufuatana na miradi, badala ya kufuatana na hatari. Unaandika ratiba nzuri yenye rangi na michoro, inaonekana ya kimkakati kwenye karatasi, lakini ni 'sanaa ya kuonekana sawa' bila kuathiri lolote kiuhalisia.

Ndio maana baadhi ya kampuni zinatumia mabilioni kwenye mfumo mpya wa kompyuta halafu wafanyakazi wanaendelea kufanya kazi kwa mtindo wa zamani, wakisubiri 'hili nalo litapita'.

Njia bora ni kubadili swali, badala ya kuuliza 'tunatangaza nini leo?', uliza 'wapi tunaweza kuanguka kimyakimya bila mtu kutambua?'

Ndipo mawasiliano yanapohama kutoka kwenye kazi ya kupamba hadi kazi ya kulinda mustakabali wa mradi mzima.

Dunia ya kazi haihitaji watu wengi wa kupiga debe. Inahitaji watu wanaoelewa hatari, wanaoongea lugha ya bosi na lugha ya kawaida wa kazini kwa wakati mmoja.

Vinginevyo mtaishia kuwa na kampuni yenye vipeperushi vizuri lakini wafanyakazi wakiwa gizani kabisa kuhusu wapi inaelekea.

Hatimaye, mabadiliko ya kidijitali hayafanikiwi kwa sababu ya seva mpya au programu ya bei ghali.

Yanafanikiwa kwa sababu watu wameelewa, wamekubali na wanaendelea na mabadiliko hayo hata bosi hayupo chumbani.

Kazi ya mawasiliano siyo kuongeza sauti, ni kuhakikisha sauti hiyo inasogeza kampuni mbele, siyo kuipamba tu iwe nzuri kwenye ripoti ya mwaka.

Mwandishi wa safu hii ni mtaalamu wa Uhusiano na Umma (PR). Anapatikana kwa namba: 0625 704 995 na kupitia email; projects@ lothmakuza.co.tz

***Mwandishi wa safu hii ni mtaalamu wa Uhusiano na Umma (PR). Anapatikana kwa namba: 0625 704 995 na kupitia email; projects@ lothmakuza.co.tz***



Na Emmanuel JACOB

# Kwa nini watumiaji wa wheelchair husukumwa?

MARA nyingi, ukitembea mtaani hasa mijini, utaona mtu aliyeketi kwenye kiti-mwendo (wheelchair), anasukumwa na mtu mwingine.

Inaonekana kama kitendo cha kutoa msaada au wema wa kawaida, lakini ukichunguza kwa undani, taswira hii inafichua ukweli mchungu kuwa tumeruhusu dhana potofu na miundombinu mibovu kumpokonya mtumiaji wa kiti-mwendo uhuru wake.

Kimsingi, kiti-mwendo hakikubuniwa ili kumfanya mtu awe tegemezi wa kusukumwa kila mahali; kilibuniwa kuwa chombo cha kumfanya mtu ajitegemee na atembee kwa uhuru wake mwenyewe.

Lakini kwa nini kila tunayemwona mjini leo anasukumwa?

Kwa wasomaji wa Gazeti la Pambazuko safu hii imeangazia baadhi ya sababu zinazosababisha jambo hili angalau kwa ufupi ambazo ni pamoja na mchanganyiko wa mazingira magumu, sababu za kiafya, au wakati mwingine, ukosefu wa uelewa wa kijamii.

Mazingira yasiyofikika; mitaa yetu imejaa ngazi ndefu, barabara zisizo na sehemu rasmi ya kushikilia (ramps), miundombinu mibovu na kando za barabara zilizoinuka mno. Katika mazingira kama haya, kujisukuma mwenyewe inakuwa vigumu.

Uchovu wa kimwili; kujisukuma mwenyewe kunahitaji nguvu kubwa ya mikono na kifua. Mtu anaposafiri umbali mrefu katikati ya mji, akiwa anatumia manual wheelchair, uchovu unamlazimu kutafuta msaada.

Hali za kiafya na majeraha; watu wenye hali kama vile kupooza mikono, kiwiliwili na miguu, ugonjwa wa mfumo wa fahamu (Multiple Sclerosis), au wale wanaouguza majeraha ya muda mfupi, wanaweza kukosa uwezo wa kutosha wa mikono au nguvu za kujisukuma.

Pamoja na kwamba kutoa msaada ni jambo la kiutu, kuna tatizo kubwa linalojitokeza mara kwa mara: watu kuwasukuma watumiaji wa



viti mwendo na wakati mwingine bila hata kuwaomba ridhaa au idhini.

Kitendo hiki kinachukuliwa na wengi kama wema, lakini katika ulimwengu wa kisasa na haki za watu wenye ulemavu, ni ukiukaji mkubwa wa mipaka ya mtu.

Kiukweli ni muhimu jamii ifahamu kumsukuma mtumiaji wa kiti mwendo hupoteza uhuru wake kujiamulia.

Unamnyima mtu haki ya kuchagua wapi aende, kwa kasi gani, na kwa wakati gani. Vilevile, humfanya mtu aonekane kama mtoto. Kitendo hiki kinajenga taswira kwamba mtu mwenye ulemavu ni dhaifu, hawezi kujifanyia maamuzi, na anahitaji "kusaidiwa" kila wakati.

Ni wakati sasa wa kubadili mtazamo wetu kama jamii. Usawa wa kweli sio tu kutoa msaada; ni kutengeneza mazingira yanayomwezesha kila mtu kujitegemea na kuheshimu utu na mipaka ya kila binaadamu.

***Mwandishi: Emmanuel Jacob, Afisa Mfiziotherapia (Mwenyekiti wa Tanzania Physiotherapy Initiative). Simu: 0765359305 Instagram: Emmanuel Jacob***

Bustani ya Sheria



Na Wakili Karim Gabriel Mussa

# Sakata la Wakili Fatma Karume – II

KATIKA sehemu ya kwanza tuliona jinsi Mahakama Kuu ilivyotupilia mbali kesi ya Ado Shaibu dhidi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wengine, lakini kabla ya kufunga jalada lake ikamsimamisha kwa muda Wakili Fatma Karume kufanya kazi za uwakili kutokana na lugha aliyotumia dhidi ya aliyekuwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Adelardus Kilangi.

Mahakama ikaagiza suala hilo lipelekwe kwenye Kamati ya Maadili ya Mawakili (Advocates Committee) ili iamue kama kweli Fatma alifanya utovu wa nidhamu.

Lakini kilichotokea mbele ya kamati hiyo kilikuwa kikubwa zaidi kuliko wengi walivyotarajia.

Lengo lake lilikuwa moja tu; kamati itamke kwamba Fatma Karume amefanya utovu mkubwa wa nidhamu na afutwe kabisa kwenye Daftari la Mawakili.

Kwa lugha nyingine, serikali haikutaka asimamishwe kwa muda tena. Ilikuwa inataka avuliwe uwakili kabisa.

Fatma aliwakilishwa na Wakili Peter Kibatala, huku serikali ikiwasilishwa na Mwanasheria Mkuu pamoja na timu ya Mawakili wa Serikali.

Ushahidi wa serikali

Serikali haikujenga kesi yake kwa yale maneno yaliyotolewa Mahakamani pekee. Ilipeleka mashahidi wanne pamoja na nyaraka mbalimbali.

Mwanasheria Mkuu alidai kwamba Fatma alimdhalilisha kwa kumuita wakili mchanga asiye na uwezo.

Alitoa maoni ya kumdhalilisha binafsi badala ya kujibu hoja za kisheria.

Alidhoofisha heshima ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, alivunja maadili ya taaluma ya uwakili.

Hata hivyo, kulikuwa na jambo jingine lililozidisha uzito wa kesi, serikali ilileta Tweets za Fatma Karume - Kamati iliwasilishwa nakala za machapisho mbalimbali ya Fatma Karume yaliyokuwa yamewekwa kwenye akaunti yake ya Twitter (X ya sasa).

Katika baadhi ya machapisho hayo aliandika maneno makali dhidi ya viongozi wa serikali, Mahakama na hata baadhi ya majaji.

Baadhi ya ujumbe huo ulionyesha kuwa; Mahakama ilikuwa ikitumika kumkandamiza, mfumo wa haki ulikuwa haukutenda haki.

Alisema kuwa alikuwa tayari kupambana kwa ajili ya utawala wa sheria hata kama angepoteza kila kitu.

Serikali ikadai machapisho hayo yalikuwa sehemu ya mwenendo unaoonyesha ukosefu wa maadili ya taaluma.

**Fatma alijibu nini?**

Kupitia Wakili wake Peter Kibatala, Fatma Karume hakukubali madai hayo. Kwanza kabisa alisema; hakuwa na imani na Kamati yenyewe.

Kwa nini? Kwa sababu, kwa mtazamo wake, baadhi ya wajumbe wa Kamati walikuwa na uhusiano wa karibu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ambaye ndiye aliyekuwa mlalamikaji.

Kwa hiyo akaamini kuwa asingepata haki, ingawa hakuwaita mashahidi wake, Fatma aliwasilisha kiapo chake cha maandishi.

Katika kiapo hicho hakurudi nyuma, aliendelea kusisitiza kwamba; Adelardus Kilangi alikuwa wakili mdogo kwa mujibu wa Roll Number za Mawakili.

Kwa maoni yake ya kitaaluma, hakuwa na uwezo wa kushika nafasi ya Mwanasheria Mkuu.

Kauli zake zilikuwa maoni ya kitaaluma, siyo matusi wala dharau, kwa kifupi, Fatma hakukanusha alichokisema. Alitetea haki yake ya kukisema.

Baada ya kusikiliza pande zote, Kamati ikaamua kwamba kabla ya kutoa hukumu ilipaswa kujibu maswali makuu matatu; Kwanza, je, akaunti ya Twitter iliyowasilishwa ilikuwa ya Fatma Karume?

Pili, kama ni yake, je, maneno aliyoyaandika pamoja na aliyoyasema Mahakamani yalifikia kiwango cha utovu wa nidhamu wa kitaaluma?

Tatu, ikiwa ni kweli alifanya kosa, adhabu ipi ilikuwa sahihi kutolewa?

Majibu ya maswali hayo ndiyo yaliamua hatma ya taaluma ya mmoja wa mawakili maarufu zaidi nchini Tanzania.

Itaendelea wiki ijayo…

***Mwandishi ni Mwanasheria na Mchambuzi wa Sheria kutoka KGM Attorneys). Anapatikana kwa namba: 0755 395 572 au Email: karimbinmussa@gmail.com***



Na Rashid MTAGALUKA

# Demokrasia haiishi kwenye sanduku la kura pekee

DEMOKRASIA hupimwa kwa vigezo vingi kuliko idadi ya kura zinazopigwa siku ya uchaguzi.

Hupimwa pia kwa namna wananchi wanavyoweza kutoa maoni yao, vyama vya siasa vinavyoweza kushindana kwa hoja, na taasisi za dola zinavyotekeleza sheria kwa haki bila kuacha maswali kuhusu usawa.

Ndiyo maana matukio ya kisiasa yaliyoshuhudiwa wiki iliyopita yameendelea kuzua mjadala mpana kuhusu mustakabali wa demokrasia nchini.

Katika miezi ya karibuni, mjadala mkubwa umejikita kwenye hatua zinazochukuliwa na vyombo vya dola dhidi ya baadhi ya viongozi na wanachama wa upinzani, huku serikali ikisisitiza kuwa jukumu lake la msingi ni kulinda usalama wa wananchi na kuhakikisha sheria zinafuatwa.

Wakati huohuo, wapo wanaohoji kama mazingira yaliyopo yanatoa nafasi ya kutosha kwa ushindani wa kisiasa na utoaji wa maoni ndani ya mipaka ya sheria. Mijadala hii imekuwa sehemu ya mazungumzo ya kitaifa na kimataifa.

Kwa mujibu wa taarifa za taasisi za kimataifa na vyombo mbalimbali vya habari, watu kadhaa wanaohusishwa na upinzani walikamatwa na kufikishwa mahakamani kwa makosa mbalimbali yanayohusiana na usalama wa taifa.

Kwa upande wake, serikali imeendelea kusisitiza kuwa hatua hizo zinachukuliwa kwa mujibu wa sheria na kwa lengo la kulinda amani na usalama wa nchi.

Hali hii inaonyesha jinsi ilivyo muhimu kwa taasisi za haki kufanya kazi kwa uwazi ili kuimarisha imani ya wananchi.

Lakini historia ya mataifa mengi inaonyesha jambo moja muhimu; amani ya kudumu haiwezi kujengwa kwa nguvu za dola pekee.

Amani hujengwa pia kwa haki, uwajibikaji na uwepo wa taasisi zinazowaaminisha wananchi kwamba sheria inatumika kwa usawa kwa wote.

Pale ambapo wananchi wanaamini kuwa mahakama ni huru, uchaguzi unasimamiwa kwa haki na vyombo vya dola vinafanya kazi kwa weledi, hata tofauti kali za kisiasa hupata nafasi ya kutatuliwa kwa njia za kisheria na za mazungumzo.

Kwa upande mwingine, ni muhimu pia kutambua kuwa hakuna demokrasia inayoweza kustawi bila utulivu. Maandamano, mikutano na shughuli nyingine za kisiasa zinapaswa kufanyika kwa kuzingatia sheria za nchi, ili kulinda usalama wa watu na mali zao.

Hivyo, wajibu wa kuheshimu sheria haupo kwa serikali pekee, bali pia kwa vyama vya siasa na wananchi kwa ujumla wake.

Aidha, takwimu za taasisi mbalimbali za kimataifa zinaonyesha kuwa nchi zenye taasisi imara za utawala wa sheria huvutia uwekezaji zaidi, hujenga uchumi imara na hupunguza migogoro ya kisiasa.

Hii inaonyesha kuwa utawala wa sheria na demokrasia si maadui; bali ni nguzo zinazopaswa kujengana.

Sasa tunapoelekea katika kipindi kingine cha ushindani wa kisiasa, Tanzania ina nafasi ya kuonyesha kuwa inaweza kulinda amani bila kupunguza nafasi ya mijadala ya kisiasa inayozingatia sheria.

Serikali ina wajibu wa kuendelea kusimamia usalama kwa haki, wakati vyama vya siasa vina wajibu wa kushindana kwa hoja na kuheshimu sheria za nchi.

Ieleweke kuwa nguvu ya taifa haipimwi kwa ukimya wa wananchi, bali kwa uwezo wa taasisi zake kusimamia tofauti za maoni kwa haki.

Demokrasia ya kweli haimaanishi kutokuwepo kwa migongano ya kisiasa; inamaanisha kuwepo kwa mfumo unaowezesha migongano hiyo kutatuliwa kwa sheria, mazungumzo na kuheshimiana.

Huo ndio msingi wa kujenga Tanzania yenye amani ya kudumu, umoja na maendeleo.

***Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com***

Habari

# Mbunge Mayeye wa ACT akaliwa kooni

Na Mwandishi WETU

MBUNGE wa Kigoma Kaskazini, Kiza Mayeye (ACT Wazalendo), amekalia kuti kavu baada ya baadhi ya wanachama kumtuhumu kuwa mienendo yake vinakwenda kinyume na maadili, nidhamu na msimamo wa chama chao.

Wanachama hao wamekwenda mbali zaidi kwa kumwandikia barua rasmi mwenyekiti wa kamati ya maadili ya chama hicho Taifa, wakiiomba ichunguze mwenendo wa mbunge huyo wakidai kuwa hauridhishi na unatia shaka kupitia Ibara ya 93(1)(a), (b) (c) na (d) ya Katiba ya ACT Wazalendo ya mwaka 2015 toleo la 2024.

Mayeye ambaye pia ni Waziri Kivuli wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Mwenyekiti wa ACT Wazalendo Mkoa wa Kigoma, anatuhumiwa kukiuka mambo matano ikiwamo kwenda kinyume na Katiba ya chama hicho ya mwaka 2015 toleo la mwaka 2024 ibara ya 76 (1) (b) na (d) ambapo anadaiwa kukiuka msimamo rasmi wa chama kuhusu bajeti kuu ya serikali.

Chanzo cha kuaminika kutoka ndani ya chama hicho, kimelieleza Pambazuko kuwa barua hiyo imeandikwa na mmoja wa vigogo ambaye anashiriki vikao vya ngazi za juu vya kitaifa.

Inadaiwa kuwa kigogo huyo tayari amewasilisha barua ya malalamiko kwa kamati ya maadili taifa ili mbunge huyo achunguzwe na kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

Sehemu ya barua hiyo inasomeka; "Kwa mujibu wa Katiba, Kiongozi wa Chama (KC) ndiye



mkuu wa sera na msemaji wa masuala ya kitaifa na kimataifa akiongoza Baraza kivuli katika kutoa msimamo wa chama kuhusu bajeti kuu ya serikali. Badala yake mbunge Mayeye alijipa jukumu la kuunga mkono bajeti hiyo bila kukihusisha chama chake.

Barua hiyo ambayo Pambazuko limeona nakala yake, inamtuhumu mbunge huyo kugomea wajibu wa michango kwa ajili ya chama kwa kiwango kilichowekwa na uongozi kwa wabunge wote pamoja na kufanya matendo yanayoweza kuharibu na kuathiri taswira ya chama.

"Tuhuma nyingine ni kukataa kuhudhuria vikao mbalimbali anavyoalikwa rasmi na viongozi wa ngazi za kitaifa sambamba na kukataa majukumu ya chama anayopangiwa na viongozi bila sababu za msingi."

"Ninaomba Kamati ya Maadili ichunguze mwenendo wa mbunge huyo unaotia shaka ikiwa ni pamoja na kujikaribisha na kukiunga mkono Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kwenda kinyume na maelekezo ya chama," inasema sehemu ya barua hiyo.

Barua hiyo ikaendelea; "Kabla ya siku ya kupitishwa kwa bajeti kuu ya serikali, chama kupitia idara ya haki za binadamu na vyombo vya uwakilishi iliwaandikia wabunge na wawakilishi kuwa msimamo wa chama katika bajeti mwaka huu ni kauli ya hapana. Hata hivyo Mayeye aliipiga kura ya kuunga mkono bajeti hiyo akiwa bungeni…"

"Aidha Julai 19, mwaka huu 2026, kupitia mitandao ya kijamii yakiwamo makundi ya whatsapp Mayeye alichapisha bango lenye picha yake na maandishi ya kumkaribisha Rais Samia Suluhu Hassan mkoani Kigoma huku akihanikiza bango hilo kwa kauli mbinu inayotumiwa zaidi na CCM ya "kazi na utu, tunasonga mbele," imesema sehemu ya barua hiyo.

Juhudi za kumtafuta mbunge huyo kwa siku mbili mfululizo hazikuzaa matunda, baada ya simu yake kuita muda wote bila kupokelewa.

Hata alipotumiwa maswali kwa njia ya simu hakuyajibu licha ya kuonyesha kuwa ujumbe huo kupitia Whatsapp ulisomwa mchana wa Ijumaa, Julai 31, 2026.

# Wanaocheza kibaokata uchi kukiona

**Na Mwandishi WETU**

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dkt. Dorothy Gwajima, amesema atawasiliana na mamlaka zote za kisheria kuhusu wanawake wanaopita na vigoma mitaani wakicheza uchi, maarufu kama kibao kata.

Ngoma hizo zimekuwa zikichezwa na baadhi ya wanawake wanaoonekana wakipita mitaani na wengine wakiandaa shughuli kwenye kumbi mbalimbali nyakati za usiku.

Wanawake hao mara nyingi huvaa vazi maarufu kama kijora ambapo wengi wao hawavai nguo za ndani na pale wanapocheza hunyanyua nguo hiyo na kucheza uchi.

Kutokana na hilo, Dkt. Gwajima ameomba wote wanaotaka kujitolea kutoa elimu ya kukabiliana na vitendo hivyo wafike ofisi za serikali za mitaa yao, kata au halmashauri waoneshe nia yao ili wapewe miongozo.

Waziri huyo ambaye amekuwa na mdahalo na vijana kila wiki kupitia mtandao wa TikTok, ametoa kauli hiyo kupitia andiko lake kwenye mtandao wa Instagram akijibu hoja ya mdau ambaye alilalamika baadhi ya vitendo vinavyoharibu maadili ya watoto na kuchochea tabia zisizofaa kwenye jamii.

"Wanawake wenzangu njooni hapa tuna ujumbe wetu kutoka kwa mwanamke mwenzangu," alianza kuandika Dkt. Gwajima huku akiainisha ujumbe wa mdau huyo.

Mdau huyo aliandika; "Mhe, shikamoo mimi naomba kwenye mdahalo wa TikTok siku uongelee hawa wamama wanaozunguka na vigoma na kuvua nguo, aiseeh, unakuta wanacheza wanatembea barabarani wanapandisha nguo juu hapo kuna watoto wanawaona…"

"Jamani wanajifunza nini? Natamani tupate vibali vya kuingia mitaani kutoa elimu hii kwa akina mama yaani mmomonyoko wa maadili tunauharibu sisi wanawake kwa kiwango kikubwa."

Akijibu ujumbe huo Dkt. Gwajima akaandika;

"Kwa ujumbe huu, nitawasiliana na mamlaka zote watakaokutwa wakusanywe kwa mujibu wa sheria wakajibu kosa lao…"

"Aidha, wote wanaotaka kujitolea kutoa elimu wafike ofisi za serikali za mitaa yao, kata au halmashauri waoneshe nia yao wapewe miongozo kwani, inawezekana na ushirikiano na jamii ni tunu muhimu sana," amesema Dkt. Gwajima.

Baada ya ujumbe huo, mchangiaji mwingine akaandika; "Hivi vigoma mbona siku nyingi malalamiko yapo? Bila kuacha wamama wanafundisha watoto tabia mbaya na zaidi sana, Watoto wanafuatilia hata kupitia simu za mkononi kwa sasa."



*Mkurugenzi wa Huduma za Afya Ustawi wa Jamii na Lishe, Dkt. Rashid Mfaume, akizungumza na waandishi wa habari Jijiji Dar es Salaam jana kuhusu kufanyika kwa Mkutano wa Kimataifa wa Huduma za Msingi za Afya utakaofanyika jijini Arusha kuanzia Septemba 9-11, 2026 na kuhudhuriwa na mataifa mbalimbali. Kushoto ni Mratibu wa Huduma za Kliniki Endelevu ya Taaluma nchini, Dkt. Pius Kagoma na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini, Ofisi ya Waziri Mkuu- Tamisemi, Roida Andusamile. (Picha na Mpigapicha Wetu).*

## Barua za Wasomaji



**Tunakaribisha barua. Tuma kupitia**

**Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba; +255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz**

### Barabara ya Njombe – Songea iangaliwe

**Mhariri,**

BARABARA ni moja ya nyenzo kubwa sana za kukuza uchumi hapa nchini. Siyo uchumi wa taifa tu, hata wa mtu mmoja mmoja unategemea sana barabara nzuri.

Maeneo tunayojishughulisha na kilimo kama ilivyo kwenye mikoa ya nyanda za juu kusini, barabara ni muhimu sana.

Naeleza haya kama msingi wa kujenga hoja yangu kuitaka serikali sasa iitupie jicho la huruma barabara kati ya Njombe na Songea.

Licha ya kuwa ni barabara muhimu kwa uchumi wa mikoa hii miwili na taifa, lakini barabara hii ni nyembamba sana na ina mashimo mengi.

Kiufupi barabara hii haina uwezo wa kuhimili mikiki ya usafirishaji inayotokana na kushamiri kwa shughuli za kilimo na uchimbaji wa makaa ya mawe hapa mkoani Ruvuma.

Kwa jinsi ilivyo, ikiendelea kutumika kama ilivyo sasa basi baada ya muda mfupi hatutakuwa na barabara yenye sifa. Naiomba serikali iiangalie barabara hii muhimu ili kuhakikisha kuwa uchumi wa maeneo haya haupati pigo.

**Juma Hassan,**
**Songea Mjini.**

### Tunateseka kuvuka Daraja la Kijazi

**Mhariri,**

SISI watembea kwa miguu katika barabara chini ya Daraja la Kijazi-Ubungo, Dar es Salaam tumekuwa tukipata shida ya kupita kwa sababu vyombo vingine vya moto kama bodaboda wanapita kwenye mistari ya pundamilia (Zebra).

Wakati mwingine unakuta hata taa hazijaruhusu na unakuta bajaji nalo limesimama kwenye eneo hilo huku likiita abiria jambo ambalo limekuwa kero kwetu.

Tunaomba askari wa usalama barabarani walifuatilie hili ili kuwachukulia hatua hawa wanaovunja sheria.

Pia tunaomba kamera za usalama zifungwe katika eneo hili ili iwe rahisi kuwakamata wanaokaidi na kutozwa faini ili iwe chanzo kizuri cha mapato ya serikali.

Serikali pia ijifunze Rwanda jinsi ya kustaarabisha miji kati ya watembea kwa miguu na vyombo vya moto.

**Noela Kapoma,**
**Kimara, Dar es Salaam.**

## Ofisi za umma ziwe na wakalimani

**Mhariri,**

WATU wenye ulemavu wa kusikia wamekuwa wakikumbana na changamoto ya kusikilizwa pale wanapohitaji huduma kwenye ofisi za umma.

Mfano wanapofika katika ofisi za umma kuanzia polisi, hospitali, mahakama na taasisi nyingine za serikali, wamekuwa wakipata changamoto ya mawasiliano kwa kuwa hakuna wakalimani au watu wenye uelewa wa kutafsiri.

Badala yake wengi wamekuwa wakikumbana na dharau, kubezwa, kucheleweshwa huduma au kuachwa wakisubiri bila msaada kwa sababu tu hawawezi kuwasiliana kwa njia ya mazungumzo ya sauti.

Binafsi nimewahi kushuhudia namna mtu mwenye ulemavu wa kusikia akidharauliwa wazi wazi katika ofisi moja ya umma.

Ninaomba serikali iwe na utaratibu wa kuweka wakalimani katika ofisi zote za umma kuanzia ngazi ya chini ili hawa wenzetu wapate haki yao ya kusikilizwa.

**Moses Philip,**
**Daraja Mbili, Arusha**


MOVE FOR DISABILITY
INCLUSION BY DESIGN 26'
WALK
with Us
29th August 2026
SPONSERED BY circleg
Kua mshiriki kwa Tshs 40,000/- Tu!
Nunua ticket yako kutumia Lipa Namba
MOVE FOR DISABILITY
6 1 2 4 6 6 1 0
INCLUSION BY DESIGN 26'
SPONSERED BY
circleg
Pambazuko

Wazo Binafsi

# Jeshi la Polisi Tanzania linahitaji IPOA




IGP Camillus Wambura

Na Sam TEMU

IPOA ni kifupi cha Independent Policing Oversight Authority, yaani mamlaka huru ya usimamizi wa Jeshi la Polisi huko Kenya.

Ni chombo cha kiraia, chenye jukumu la kuchunguza vifo, majeraha na utovu wa nidhamu vinavyotokana na vitendo vya askari wa Jeshi la Polisi.

Wachunguzi wake siyo askari na hawako chini ya mkuu wa jeshi hilo, wala Wizara ya Mambo ya Ndani; wengi wanasema IPOA ni chombo kilichozaliwa kutoka kwenye damu, hili ni somo kwetu Tanzania.

Kenya walipata matukio makubwa ya mauaji, wakaunda tume, ripoti ikatoka, ikazaa sheria na chombo, lakini sisi Tanzania tumepata mauaji, tumeunda tume, ripoti imetoka, na hadi sasa tunaelezwa kuwa iko ikisubiri hatua zingine.

Juni 2025, kijana wa Kenya aitwaye Albert Ojwang aliingizwa Kituo Kikuu cha Polisi Nairobi akiwa anatembea na akiongea kwa simu, lakini alitoka pale hajitambui, na akafariki baadaye.

Simulizi ya awali ilikuwa alijiumiza mwenyewe. Kama kusingekuwa na IPOA simulizi ingefia hapohapo, lakini haikufa.

Mwaka mmoja baadaye, aliyekuwa mkuu wa kituo na maofisa wengine watano wa polisi walisimamishwa kizimbani kwenye Mahakama Kuu.

Katika kesi hiyo, Mahakama iliambiwa ushahidi kwamba mfumo wa kamera za CCTV 'ulifomatiwa' kwa makusudi ili kuficha ushahidi, na fundi aliyefanya kazi hiyo ametoa ushahidi akiwa amelindwa.

Kilichofanya tofauti kati ya kifo kilichozikwa na kifo kilichofika mahakamani ni chombo kimoja ambacho ni IPOA.

**Chimbuko lake**

Hii ndiyo sehemu inayotuhusu sisi zaidi, kwa sababu Kenya walianzia pale tulipo sasa. Baada ya uchaguzi mkuu wa 2007, vurugu ziliua zaidi ya watu 1,000.

Mwezi Februari 2008, tume ya uchunguzi wa vurugu za baada ya uchaguzi iliundwa, ikijulikana kama Tume ya Wako.

Tume hiyo ilichunguza pia jinsi polisi walivyoshughulikia vurugu hizo, na miongoni mwa mapendekezo yake makuu yalikuwa kuundwa kwa vyombo viwili vya uwajibikaji.

Mwaka 2009, serikali ikaunda kikosi kazi cha kitaifa cha mageuzi ya polisi kilichoongozwa na Jaji (mstaafu) Philip Ransley. Kikosi hicho kilimaliza kazi ndani ya siku 90, jambo lililoshangaza wengi.

Ransley ndiye aliyependekeza waziwazi kuundwa kwa IPOA kama chombo cha kiraia cha kusimamia polisi, kikiwa na mamlaka ya kupokea na kuanzisha uchunguzi, kukagua matumizi ya fedha ya polisi, na kufuatilia uchunguzi wa polisi wenyewe.

Mwaka 2010, mapendekezo ya Ransley yakaingizwa kwenye Katiba Mpya ya Kenya, ambayo iliweka misingi ya kikatiba ya utendaji wa Jeshi la Polisi.

Mwaka 2011, Bunge likatunga Sheria ya IPOA, Na. 35 ya 2011, sasa Sura ya 88 ya Sheria za Kenya. Sheria hiyo hiyo ya polisi pia ikaunda kitengo cha mambo ya ndani cha polisi wenyewe.

Inaendelea Uk. 33

# Jeshi la Polisi...

Inatoka Uk. 32

Kinachofanya IPOA kifanye kazi ni vipengele vinne, ambavyo ni pamoja na sheria yake yenyewe kwamba chombo hicho hakiko ndani ya Jeshi la Polisi wala ndani ya Ofisi ya Rais wa Kenya. Kina uhai wa kisheria unaojitegemea.

Pili, fungu lake la bajeti linaratibiwa na wenyewe na kuwajibika kutoa taarifa kwa Bunge, siyo kwa waziri pekee.

Tatu, kina wachunguzi wa kiraia wenye mamlaka ya kuingia kituo cha polisi, kukagua eneo la tukio, na kuchukua vielelezo.

Ndiyo maana kwenye kesi ya Ojwang, wachunguzi wa IPOA walikuwa tayari kituoni wakati fundi wa CCTV alipofika.

Nne, na hii ndiyo kubwa kuliko zote; wajibu wa kisheria wa kuarifu. Kifungu cha 25 cha Sheria ya IPOA kinataka polisi waiarifu mamlaka kwa maandishi ndani ya saa 24 kila kunapotokea kifo au jeraha zito linalotokana na kitendo cha polisi.

Sheria ya kuzuia mateso ya 2017 nayo inamtaka mkuu wa kituo kuiarifu mamlaka pale tuhuma za mateso zinapotolewa.

Hata hivyo, kuna changamoto mbalimbali zinazokakibili chombo hiki ikiwa ni pamoja na mamlaka kutokutekeleza sawasawa sharti la kuarifu.

Utafiti wa wataalamu unaonyesha kuwa taarifa kutoka polisi hupokelewa mara chache sana. Hata pale sheria inapowataka wafanye hivyo ndani ya saa 24.

Aidha, wakati mwingine IPOA hufika eneo la tukio kwa kuchelewa na kukuta ushahidi umeshaharibiwa na mnyororo wa uhifadhi umevunjika.

Kwa mfano, watu 62 waliuawa kwenye maandamano ya mwaka 2024, na miaka miwili baadaye, IPOA yenyewe ilitangaza kuwa ni kesi tatu tu kati ya 62 zimefika mahakamani. Nyingine 46 bado ziko kwenye uchunguzi.

Human Rights Watch inasema watu 26 wa maandamano hayo bado hawajulikani walipo. Ukijumlisha matukio matatu ya maandamano, IPOA ina vifo 127 kwenye jalada lake.

Changamoto nyingine ni kuyumba kwa baadhi ya mashauri mahakamani. Kwa mfano, uchunguzi wa kifo cha Rex Masai, mmoja wa kwanza kuuawa mwaka 2024, mawakili wa utetezi wamehoji ubora wa ushahidi uliokusanywa, na kiongozi mmoja wa upinzani ameonya hadharani kwamba ofisa anayehusika anaweza kuachiwa siyo kwa kuwa hana hatia, bali kwa sababu ushahidi haukukusanywa ipasavyo.

**Kwa upande wa Tanzania**

Tume ya Jaji Mstaafu Mohamed Chande Othman iliwasilisha ripoti Ikulu Aprili 23, 2026, ikithibitisha watu 518 walifariki, wengi kwa risasi.

Kati yao wapo watoto 21 na watu 245 hawajulikani walipo. Familia 39 ziliieleza Tume kwamba ziliona miili ya wapendwa wao kwenye vyumba vya kuhifadhia maiti kabla haijatoweka.

Jiulize, ni polisi wangapi wanachunguzwa? Kesi ngapi ziko mahakamani? Nani anafuatilia? Fidia ipo?

Hakuna anayejua, kwa sababu hakuna chombo kinachohesabu, na ripoti iliyohesabu haijafunguliwa. Tofauti kati ya nchi hizi mbili siyo kwamba Kenya hawaui, ni kwamba Kenya wanahesabu, wanaandika, na wanalazimika kujieleza.

Tanzania ingehitaji nini hasa? Siyo maneno matupu, ni vitu vinne vinavyoweza kuandikwa kwenye muswada kesho.

Tanzania pia tunahitaji chombo huru chenye sheria yake, kisicho ndani ya Jeshi la Polisi wala Ofisi ya Rais, bajeti inayojitegemea na kuwajibika kwa bunge.

Wachunguzi wa kiraia wenye mamlaka ya kuingia kituo cha polisi bila idhini ya mkuu wa kituo, na sharti la kisheria kwamba kila kifo au jeraha zito linalotokana na kitendo cha polisi liarifiwe ndani ya saa 24, likiwa na adhabu kwa asiyearifu.

Kwa sasa tuna Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora Tanzania (THUB) - ipo kikatiba, lakini haina mamlaka ya kushtaki, mapendekezo yake siyo ya lazima, na wajumbe wake huteuliwa na rais.

Kwa sasa, malalamiko dhidi ya askari hushughulikiwa ndani ya jeshi lenyewe.

Kenya hawakupata IPOA kwa sababu ni watu wema kuliko sisi, ni kwa sababu baada ya vifo zaidi ya 1,000, taifa lilikataa ripoti ya tume ambayo haikuishia kwenye kabati, yakafanyika mageuzi.

Sam Temu anajitambulisha kuwa ni mchambuzi huru wa siasa safi na uongozi bora.

Habari

# Washitukia vyama mchakato Katiba Mpya

Na Mwandishi WETU

WADAU mbalimbali wameonyesha wasiwasi wa mchakato wa kuandika Katiba Mpya kutekwa na wanasiasa na kuonya kuwa hilo linaweza kusababisha mchakato huo kuvurugika tena.

Kinachowashitua wadau hao ni mkutano uliotishwa na Rais Samia Suluhu Hassan wiki iliyopita na kuwahusisha viongozi wa vyama vya siasa, huku taarifa zilizotoka katika mkutano huo zikibainisha kuwa pamoja na mambo mengine, ulijadili suala la maridhiano kuelekea marekebisho ya Katiba.

Wasiwasi huo ni moja ya uthibitisho kuwa lipo kundi la Watanzania ambalo sasa limeingiwa shaka kwa wanasiasa kusimamia masuala makubwa na ya msingi kwa taifa.

Wadau waliozungumza na Pambazuko wameeleza kuwa kuwaachia wanasiasa mchakato huo ni kupoteza muda na raslimali za nchi, badala yake wameshauri mchakato huo uhusishe makundi mbalimbali ya kijamii, na kusimamiwa na watu wenye uzoefu na wanaoaminika kwa jamii.

Mbali na hilo, wamesema yatakuwa ni makosa makubwa kulitumia Bunge la sasa ambalo wamedai kuwa linaonekana kuwa ni la chama kimoja, kulipa uwezo na majukumu ya kuwaamulia wananchi Katiba ya kuongoza Taifa lao.

Akizungumza na Pambazuko mwishoni mwa wiki, Mhadhiri mstaafu wa Sayansi ya Siasa wa Chuo Kikuu cha Dare salaam (UDSM), Balozi Dkt. Benson Bana, ingawa anapongeza hatua ya Rais Samia Suluhu Hassan kukutana na vyama 18 vya siasa, lakini kati yake ukiondoa Chama Cha Mapinduzi (CCM), ACT Wazalendo, na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) ambacho hakikuhudhuria, vingine vilivyosalia havijawahi kufanya kazi hasa ya siasa ingawa vimeandikishwa kwenye daftari la Msajili wa Vyama vya Siasa.

Dkt. Bana alitoa angalizo hilo wakati akizungumza na Pambazuko siku moja baada viongozi wa vyama 18 kukutana na Rais Samia Ikulu, Dar es Salaam, Julai 30, 2026.

Pamoja na mambo mengine walizungumzia maridhiano, mageuzi ya kisiasa, uchumi, huduma za jamii, ajira, uwekezaji na ulinzi wa amani ya nchi.

Pia taarifa ya Ikulu iliyosainiwa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Bakari Machumu, ilisema serikali ya Rais Samia itaendeleza maridhiano ya kisiasa kuelekea hatua za maboresho ya Katiba kwa kuzingatia sheria na taratibu za nchi.

Dkt. Bana ameshauri kuwa ili kupata Katiba itakayokubalika na wengi ni vyema mchakato wowote wa maridhiano na Katiba Mpya uwashirikishe watu wenye busara, wazoefu na wanaokubalika na makundi yote kwenye jamii.

Alipotakiwa kuwataja watu hao, Dkt. Bana alibainisha kuwa Waziri Mkuu mstaafu, Joseph Warioba, Mzee Joseph Butiku, Profesa Anna Tibaijuka na Rais (mstaafu) Jakaya Kikwete, ni kati ya watu ambao wanaweza kuwaleta pamoja Watanzania kujadili Katiba Mpya.

Mwanazuni huyo aliwataja watu wengine maarufu kuwa ni pamoja na marais wastaafu wa Zanzibar; Abeid Aman Karume, Dkt. Mohammed Ally Shein na mawaziri wakuu wastaafu; Fredrick Sumaye, Kassim Majaliwa na Makamu wa Rais wa zamani, Dkt. Philip Mpango.

Aidha, Dkt. Bana ametahadharisha kuwa kamwe mchakato wowote wa maridhiano usikiache nje Chadema kwa sababu ni ukweli usiopingika kuwa ndicho chama kikubwa cha pili nchini kwa nguvu, pamoja na kuwa chama kikubwa cha upinzani nchini.

“Hivi vyama vingine hata itikadi yao haijulikani, chama cha siasa lazima kiwe na itikadi. Waulize chama kimoja kimoja, itikadi yao iko wapi? Chama cha siasa lazima kiwe na presence (uwakilishi), kiwe na matawi, kiwe na sura, kiwe na structure (muundo)...”

“Hivi vyama vingine, ingawa vimeandikishwa kwenye daftari la Msajili, lakini havijawahi kufanya kazi ya siasa wala kuonekana vijijini vikipeperusha bendera...”

“Tuna Katiba iliyopo sasa hivi, ina upungufu, kwa hiyo nayo siyo bora, Watanzania wanataka Katiba bora. Ikiwa mpya ikawa bora ni vizuri zaidi...”

Inaendelea Uk. 35

# Washitukia vyama...

Inatoka Uk. 34

"Ikiwa mpya isiwe bora ni jambo jingine. Sasa Katiba bora hiyo ni hitaji. Na bahati nzuri CCM kimeiweka kwenye ilani yake kwamba kitatupa katiba bora, Katiba Mpya..."

"Hilo ni jambo jema, lakini mchakato wa kufikia hapo lazima uwe shirikishi; vyama vya siasa ni sehemu ndogo kwani Katiba ni ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lazima tushiriki. Makundi yote yashirikishwe - wakulima, wafanyakazi, wakuna nazi, wavuvi, wafugaji, wajasiriamali, wafanyabiashara, wadogo kwa wakubwa. Kila kundi lishiriki, utaratibu wa kushiriki haujatushinda," anasema Dkt. Bana.

Kwa upande wake, mwanasheria nguli nchini, Boniface Mwabukusi, amesema vyama vilivyokutana na Rais Samia wiki iliyopita ni kiinimacho na haviwezi kuipatia nchi Katiba Mpya.

Alisema viongozi wa vyama hivyo ndiyo waliokaa pamoja na chama tawala wakakubaliana kuingia kwenye uchaguzi mkuu na baadaye kuutangazia umma kwamba uchaguzi huo wa Oktoba 29, 2025 ulikuwa huru na haukuwa na dosari.

Hivyo, anasema hata viongozi wake hawawezi kuaminika kwa namna yoyote katika suala linalohusiana na mchakato huo kwa sababu ule uchaguzi ambao walisema ni wa haki na salama, ulisababisha vifo vya mamia ya Watanzania kama ambavyo serikali yenyewe imekiri kupitia tume iliyoundwa na Rais Samia.

Wakili Mwabukusi, ambaye katika mahojiano hayo alisisitiza kuwa anazungumza kama mtu binafsi na siyo kwa niaba ya Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS) ambacho yeye ni rais wake, alibainisha kuwa mchakato wowote unaohusu maridhiano na Katiba Mpya, lazima uzingatie ukweli, haki na uwajibikaji kwa yaliyotokea kwenye uchaguzi mkuu wa Oktoba mwaka jana.

"Haya mambo hayahitaji ujanjaujanja kana kwamba hakuna kilichotokea. Amani, maridhiano na mabadiliko yanafanyika na wale walioguswa, ikiwa watu hawajisikii kuwa na shida, hawatashiriki kutatua na wala tatizo halitaondoka kwa sababu wao ni ama ndiyo tatizo lenyewe au sehemu ya tatizo..."

"Huwezi kuanza mchakato mwingine wowote bila ukweli kudhihirika, hatujasikia hivi vyama vilivyokwenda Ikulu kuwa vina malalamiko wala havijaumizwa na lolote," alisema wakili huyo nguli.

Kwa upande wake, Jukwaa la Katiba Tanzania (Jukata), limeshauri Rais Samia amwagize Waziri wa Sheria na Katiba kupeleka bajeti ya dharura bungeni kwa ajili ya kugharamia mchakato wa kukamilisha uandikwaji wa Katiba Mpya.

Akizungumza na Pambazuko mwishoni mwa wiki iliyopita, Mwenyekiti wa Jukata, Dkt. Ananilea Nkya, alisema suala hilo linatakiwa kufanyika haraka ili kukidhi kalenda ya uchaguzi wa serikali za mitaa 2029 na uchaguzi mkuu wa 2030.

Alisema Katiba Mpya ndiyo pekee itakayoleta maridhiano ya kweli, tofauti na utaratibu wa kukaa na vyama vya siasa vinavyotiliwa shaka na wananchi. "Kinachotia doa maridhiano haya ni kutokuwepo kwa suluhu ya matukio ya watu kutekwa na kikundi kisichojulikana, kupotea," alisema.

Naye mwandishi mbobevu mstaafu na mshauri mwelekezi wa habari na jinsia, Rose Haji, amesema Tanzania inahitaji maridhiano kama aliyoyafanya Rais wa zamani wa Afrika ya Kusini, Nelson Mandela na serikali ya makaburu katika kuponyesha majeraha ya watu kwa kusameheana kuvumiliana na kusonga mbele. Amesema jambo hilo linafanana na zile R4 za Rais Samia alizozitangaza siku chache baada ya kuchukua madaraka baada ya kifo cha Rais John Magufuli mwaka 2021.

"Ingawa sio lazima kufuatisha mchakato wote alioufanya Rais Mandela, lakini angalau tuuchukue kama mfano. Wananchi waruhusiwe watoe maoni yao kama walivyofanya kwa tume ya kuchunguza machafuko ya Oktoba 29, 2025 ya Jaji mstaafu Othman Chande.

"Mfano mwingine ni ule wa Rwanda, baada ya mauaji ya kimbari ya mwaka 1994, walikaa wakatengeneza mahakama ya jamii iliyojulikana kama 'Gachacha' kwa lugha ya kwao ambapo watu waliona wamekosana, wanasameheana, wanaponya majeraha na wanasonga mbele na kama kuna mhalifu sheria inachukua mkondo wake..."

"Lakini hapa kwetu yote mawili hayajafanyika, aliyekosa na aliyekosewa hatumjui. Hiyo ripoti ya Jaji Chande hatuijui, sasa kuridhiana na vyama vya siasa peke yao nasema hapana, kwanza vinajua nini?" anahoji Rose Haji.

# Habari katika picha

*Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akizungumza na viongozi wa vyama vya siasa 18, Ikulu jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Picha na Ikulu.*





*Rais Samia Suluhu Hassan akiteta jambo na Mwenyekiti wa Chama cha AAFP, Said Soud Said baada ya mkutano na viongozi wa vyama vya siasa nchini, Ikulu jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. (Picha na Ikulu)*



*Baadhi ya viongozi wa vyama vya siasa nchini walioshiriki kwenye mkutano na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Ikulu jijini Dar es Salaam, Julai 30, 2026. (Picha na Ikulu)*



*Mbuzi wakizurura katika barabara Kawawa eneo la Msimbazi. Hawa wanavunja sheria za jiji zinazozuia mifugo kurandaranda mitaani na kusababisha kero kwa watumiaji wa vyombo vya moto, jijini Dar es Salaam jana. (Picha na Mpigapicha Wetu).*



*Mfanyabiashara ya karanga za kuchemsha akiziandaa kwa ajili ya kupeleka sokoni kuuza kama alivyokutwa na Mpigapicha Wetu, Fidelis Felix jana. Karanga hizo huuzwa kwa kutembezwa na vijana mitaa ya Jiji la Dar es Salaam.*

# TVNL 2026, hii sio ya kukosa

Na John Marwa

MOJA ya burudani ya mchezo ambao unazidi kushika kasi kwenye masikio na macho ya wapenda michezo licha ya uwepo wake muda mrefu ni Ligi ya Taifa ya Mpira wa Wavu Tanzania (TVNL 2026) ambayo inaanza kuchukua nafasi Septemba 3, katika viwanja vya Mwembe Yanga, Temeke jijini Dar es Salaam, kwa mzunguko wa kwanza.

Ni mchezo ambao umekuwa kivutio cha makundi mbalimbali kwa namna ambavyo umekuwa sehemu ya kutoa burudani, ajira na fursa kwa vijana, klabu za vyuo na taasisi za serikali na mashirika binafsi.

Jumla ya klabu 24 zitashuhudiwa zikimenyana kusaka ubingwa wa msimu huu katika Ligi ya Wanawake timu 10 huku wanaume zikishiriki klabu 14.

Kwa upande wa wanaume klabu ya Chuo Kikuu cha Kampala (KIUT) ndio Mabingwa watetezi ambapo watakuwa na kibarua kizito kubakisha taji hilo dhidi ya miamba kama Magereza, Jeshi Stars, High Voltage, Bamdari, Genesis, Nyika.

Wakati kwa upande wa Wanawake Tanzania Prisons wana kibarua kingine cha kuendelea kuonyesha umwamba kwa kuutetea ubingwa wao mbele ya Bandari, Korosho Queens, KIUT, JKT na Jeshi Stars.

Ni msimu unaotarajiwa kuwa na msisimko mkubwa kutokana na ukuaji wa kasi wa Ligi hiyo sambamba makampuni mbalimbali, kama Vodacom, GSM Beverages, Dames Engineering Limited na 26 Liquor, kuanza kuidhamini jambo ambalo linatoa chachu na ari ya kupambana zaidi.

Michezo yote kwa Ligi ya Wanawake na Wanaume inapigwa pale Mwembe Yanga huku ikioneshwa mubashara kupitia Azam Sports.



Na Anti MSHAURI







# Weka akiba hata kwa kipato kidogo

HABARI msomaji wangu wa safu hii ya uhusiano ili tujifunze pamoja kuhusu maisha.

Wiki hii nitaeleza umuhimu wa kujiwekea akiba hata kama una kipato kidogo, kwani watu wengi hushindwa kuweka akiba wakisema kuwa kipato chao ni kidogo.

Lakini ukweli ni kwamba ni mtu unaweza kuweka akiba bila kujali unaingiza kiasi gani cha fedha. Suala la kuweka akiba ni la kibajeti na halihusiani kabisa na kiasi cha fedha mtu anachopata.

Mtu unaweza kuweka akiba kwa kiasi chochote cha fedha unachipata. Ukipata nyingi utaweka akiba kubwa na ukipata kidogo utaweka akiba kidogo.

Lakini kwa kuwa akiba haiozi, basi hata hicho kidogo unachoweka itafika siku kitakuwa kikubwa.

Ili kufanikisha suala la kuweka akiba na kuikuza ni muhimu kuwa na nidhamu ya matumizi.

Wapo pia wanaofanya matumizi yao ya siku, wiki na hata mwezi bila kufanya hesabu au kujiwekea akiba ambayo itawafaa baadaye.

Lakini jambo jingine la kuzingatia ni kuwa akiba siyo fedha ya matumizi kwa sababu wapo watu ambao wanaweka akiba, ingawa wakipata shida kidogo wanaitumia shida jiyo kutatua shida zao.

Unaweza kuanza leo, hata kwa Shilingi 500, baada ya muda utafika mbali.

Kikubwa cha kuzingatia ni kuwa akiba siyo fedha inayobaki baada ya matumizi, bali akiba inapaswa kuwa fedha ya kwanza kutolewa kwenye kipato chako kabla ya matumizi mengine.

Mara upapopata kipato hicho toa kiasi ulichopanga kama akiba na fedha inayobaki baada ya kutoa akiba ndio ipangiwe matumizi mengine.

Usisubiri kuwa upate fedha nyingi ndio uanze kuweka akiba kwa sababu kwa asili ya binadamu hakuna fedha nyingi. Hivyo kila kiasi cha fedha unachopata kinafaa kuanza kuweka akiba.

Usiweke fedha zote pamoja. Kuwa na akaunti ya matumizi na nyingine ya akiba.

Usichanganye fedha za matumizi na fedha za akiba ili kujiondolea ushawishi wa kutumia fedha uliyoiweka akiba.

Lakini pia jaribu Changamoto ya Wiki 52; Hii inafanya akiba iwe ya kufurahisha. Wiki ya kwanza weka Shilingi 1000, wiki ya pili weka Shilingi 2000, na ongeza Shilingi 1,000 kila wiki. Mwaka ukiisha utakuwa na zaidi ya Shilingi milioni 1.3. Unaweza kuanza na Shilingi 500 kama Shilingi 1,000 ni nyingi.

Acha matumizi yasiyo ya lazima na katika hili tambua matumizi yasiyo ya msingi; soda kila saa, data ya kupita kiasi. Chagua kitu kimoja cha kukata na ile pesa uhamishe kwenye akiba. Ukiacha soda ya Shilingi 1,000 kwa siku, utaweka Shilingi 30,000 kwa mwezi.

Akiba ni kinga ya maisha ambayo inakulinda wakati wa dharura, inakusaidia kufikia malengo, na inakupa amani.

Tukutane wiki ijayo.

***Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.***

# Namna ya kupangilia 'tennis shoes' na sketi

VAZI la sketi na chini ukapigilia viatu aina ya tennis, ni mtindo wa kisasa unaovuma hivi sasa.

Ili uonekane wa kisasa zaidi ndani ya vazi hili, ni muhimu uzingatie aina ya sketi na blauzi, crop top au shati.

Hapa chini nimekuwekea maelezo na mifano ya namna ya kuvaa ili uonekane nadhifu zaidi.

**Sketi fupi**

Huu ni mtindo wa kisasa na wa ujana zaidi.

* Hapa unatakiwa kuvaa t-shirt au crop top na uchague tennis shoes nyeupe au zenye rangi nyepesi. Unaweza kuongeza soksi fupi kwa mvuto zaidi.

* Vazi hili linafaa kwa matembezi au outing

Sketi ndefu

Mtindo huu unatoa muonekano wa heshima zaidi.

* Unatakiwa kuchagua sketi laini ili kuendana na viatu.

* Chagua tennis shoes simple nyeupe au nyeusi, juu unaweza kupigilia na blauzi au t-shirt.

* Vazi hili linafaa kwa kazi zisizo rasmi, kanisani na outing za heshima.



# Tumia kahawa na maziwa kwa ngozi nyororo

MCHANGANYIKO wa kahawa na maziwa ni njia nzuri ya kuondoa seli zilizokufa na baadaye hulainisha na kufanya ngozi kuwa nyororo.

Pia mchanganyiko huo husaidia kutoa madoa na kuchochea mzunguko wa damu kwenye ngozi.

**Jinsi ya kuandaa;**

*Weka kijiko kimoja cha unga wa kahawa kwenye bakuli na kiasi kidogo cha maziwa.

*Koroga pamoja hadi upate mchanganyiko mzito kiasi.

*Paka usoni au mwilini, sambaza huku ukisugua taratibu kwa mzunguko.

*Acha ikae kwenye ngozi kwa muda wa dakika 10 hadi 15.

*Kisha jisafishe kwa maji baridi au ya vuguvugu halafu jikaushe kwa kitambaa safi. Fanya hivi mara tatu kwa wiki kwa matokeo mazuri zaidi.





# Diamond, Zuchu 'aibu utaona wewe'

**Na Mwandishi WETU**


WIKI chache baada ya wasanii, Diamond na Zuchu kutangaza kuachana, hatimaye wasanii hao wameonekana wakiwa pamoja kwenye sherehe ya maandalizi ya ujio wa mtoto wao (baby shower).

Wakati sherehe hiyo ya baby shower ikiendelea nyumbani kwa Zuchu, Mbezi Beach, jijini Dar es Salaam wiki iliyopita, ghafla akaibuka Diamond na kwenda kumkumbatia Zuchu.

Hali hiyo iliibua gumzo mtandaoni huku wachangiaji wengi wakisema watafícha wapi sura zao wakati walishabikia wawili hao walipotangaza kuachana.

Diamond alipotakiwa kwenda kumtunza mkewe, alitoa dola za Marekani zenye thamani ya zaidi ya Shilingi milioni 70.

"Hii dola nimetoa haraka haraka tu kwa kuwa nimeshtukizwa, lakini Zuchu anastahili zawadi nzuri zaidi kwani ataniletea zawadi ya mtoto wa kike," amesema Diamond.




# Shoo ya Tyla ilivyofutwa Nigeria

**Na Mwandishi WETU**

ZIARA ya staa wa muziki kutoka Afrika Kusini, iliyopangwa kufanyika nchini Nigeria haitakuwepo tena kufuatia uamuzi wa kuiondoa Lagos kwenye ratiba yake ya "APop Tour".

Hatua hii imekuja baada ya wimbi kubwa la mashabiki na wananchi wa Nigeria kutangaza kutompa ushirikiano nchini humo. Ghadhabu za Wanigeria zimechochewa na kero ya muda mrefu dhidi ya vitendo vya chuki kwa raia wa kigeni (Xenophobia) nchini Afrika Kusini, pamoja na operesheni za kurudishwa makwao kwa raia wanaodaiwa kuishi bila nyaraka halali. Maandamano yamekuwa yakiendeshwa na wananchi nchini Afrika Kusini, wakilalamikia ukosefu wa ajira wanaodai unachangiwa na ongezeko la wageni.




# 'Happy Birthday' Nguvu Moja

Na John Marwa

KUTOKA mitaa ya Msimbazi, Kariakoo, Dar es Salaam ilipo ngome ya biashara Afrika Mashariki, alizaliwa mtoto Malkia, wahenga wakambatiza Sunderland.

Hata hivyo, kizazi kipya kinatamba na jina lake la maajabu kutoka mbuga za wanyamapori - mfalme wa mwitu, Simba SC; jina linalotisha katika mawindo ya soka Afrika.

Agosti 8, 1936 alizaliwa mtoto huyu mwenye roho ya nguvu moja, ni miaka 90 sasa, klabu yenye kutoa uhalisia wa Mnyama Simba mawindoni kwa jinsi ambavyo amekuwa akizichanga karata zake.

Klabu yenye nguvu na ubora Afrika Mashariki na Kati na kusini mwa Jangwa la Sahara. Mvuto wa kikongwe huyu siyo tu unyama wake dimbani, siyo tu mitandaoni wala siyo ushawishi wake ndani na nje ya uwanja, bali ni nguvu ya kuishinda mioyo ya mamilioni ya wapenda kabumbu ulimwenguni.

Tamasha la 'Simba Day' ambalo limekuwa utambulisho wa Simba kukutana kwa pamoja ndani ya mbuga ya Lupaso, kula na kunywa chakula cha hisia, moyo na mahaba kwa kuwatambulisha Simba wapya, wale wanaoibeba bendera ya Lunyasi katika msimu husika.

Hii ndio klabu iliyofika mara nyingi zaidi hatua ya robo fainali Ligi ya Mabingwa Afrika (CAFCL) kutoka Afrika Mashariki.

Ni moja ya silaha ya kujivunia kwa mashabiki wa Simba ambao wanashikilia tuzo ya mashabiki bora barani Afrika.

Mnyama siyo tu anavutia kizazi kipya, bali ni roho ya Tanzania katika medani za soka la Afrika, mara nyingi bendera inapokuwa mabegani mwa wekundu wa msimbazi, hata mashaka kwani ndio michezo anayoipenda muhenga wa kandanda la nchi.

Mohamed Dewji ndio jina lenye thamani kubwa katika kila hatua za mafanikio ya ndani ya uwanja kiuchumi kama ambavyo ni kinara wa mabilionea wa Tanzania, kwake Simba ni mishipa ya furaha ipelekayo burudani ya kabumbu moyoni mwake.

Jumamosi nchi itasimama kuandika historia ya Mfalme wa Mwitu mwenye makazi yake katika mbunga ya biashara na mawinga, kusherekea miaka 90 tangu kuanzishwa kwake. Heri ya kumbukizi ya kuzaliwa Simba SC.



# Hersi kutimiza ahadi zake?



Hersi Said

**Na Mwandishi WETU**

NI Hersi tena hivi ndivyo unavyoweza kusema baada ya wanachama wa Klabu ya Yanga kumchagua tena Hersi Said kuwa rais wa klabu hiyo kwa miaka minne ijayo.

Hersi ambaye ni msanifu wa majengo – kitaaluma, amekuwa kipenzi cha wanachama na mashabiki wengi wa Yanga kwa uongozi wake kwani katika kipindi chake amefanikiwa kuipatia klabu hiyo kongwe mataji matano ya Ligi Kuu Tanzania Bara, mataji manne ya FA na Ngao ya Jamii nne.

Kimataifa, Yanga walifanikiwa kufikia hatua ya fainali ya Kombe la Shirikisho CAF msimu wa mwaka 2022/23, chini ya kocha Nasreddine Nabi na ikawa klabu ya kwanza Tanzania kufika hatua hiyo ambapo walipoteza dhidi ya USM Alger kwa faida ya bao la ugenini.

Hersi amefanikiwa kuwa Rais wa Vilabu Afrika pia amekuwa mjumbe katika kamati ya FIFA ya mashindano ya wanaume.

Chini ya uongozi wake, amefanikiwa kuongeza mapato ya klabu hiyo ambayo ilikuwa ikipitia ukata mkubwa na kuanza kutembeza bakuli, lakini kwa sasa “mambo mswano” kwani wanatengeneza fedha kupitia mikataba mbalimbali ya wadhamini, viingilio vya mechi, mauzo ya jezi pamoja na tamasha la Siku ya Mwananchi ambalo hufanyika kila mwaka mwanzoni mwa msimu.

Hersi Said aliingia kwenye nafasi hiyo mwaka 2022 baada ya klabu hiyo kufanya mabadiliko ya katiba.

Mfupa mgumu wa Hersi mpaka sasa ni ahadi yake ya ujenzi wa uwanja wa kisasa ambao aliitoa tangu anashika wadhifa huo mwaka 2022, lakini hadi sasa inaonekana kumshinda awamu hii pia amewaahidi tena Yanga kuwa atatimiza ahadi yake hiyo.

Swali kubwa ni moja;  je, sasa atatimiza ahadi hiyo ndani ya kipindi chake cha uongozi?

*GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.*

TAMPA
TANZANIA MEDIA PRACTITIONERS ASSOCIATION